**Watoto** 981 wilaya moja wapata ujauzito kipindi cha miezi sita

UKURASA 3



**Mashahidi** 10 wa Jamhuri na vielelezo 10 leo kuanza kujenga kesi ya Sabaya

UKURASA 4


Nipashe Spotika

NYOTA A. MASHARIKI WALIOTIKISA EURO 2020

ISIKUPITE

UKURASA 11

Nipashe

Jumatatu Julai 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580646

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Chanzo mauaji D'salaam chatajwa

•**MASHUHUDA** baa wafunguka kila kitu...

*Endelea ukurasa 2*



Mchoro wa picha ukionyesha mfano alivyoua.



Mchoro wa picha ukionyesha mfano alivyojiua.

## Mambo sita kuhusu tozo miamala simu

UKURASA 4



## CHADEMA yagoma kuwawekea dhamana viongozi wake Mwanza

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA QUEENS WAHITAJI MECHI TATU KUJIFUA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mjumbe wa Bodi ya Uwekezaji ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA Africa Region) na Mbunge wa Bunge la Afrika Kusini, Lechesa Tsenoli (katikati), akichangia jambo wakati wa kikao cha bodi hiyo, Nairobi nchini Kenya, jana. Kushoto ni Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid na Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chanzo mauaji baa Dar chatajwa

**Na Elizabeth Zaya**

CHANZO cha mfanyabiashara Alex Koroso (37), kumuua fundi magari anayefahamika kwa jina moja la Gift, katika baa ya Lemax, Sinza wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, kisha naye kujiua kimeelezwa kuwa ni ulevi kupita kiasi.

Pia dalili za matumizi mabaya ya silaha anayoimiliki kihalali zilionekana tangu Juni 13, mwaka huu, siku ya kumbukumbu yake ya kuzaliwa ambayo moja ya keki zake iliandikwa 'Happy birthday Alex' na katikati kukiwa na picha ya bastola.

Mashuhuda wa tukio hilo walidai kuwa Alex alianza kufanya vurugu kwenye baa hiyo tangu asubuhi, akiwa amelewa baada ya kukesha katika baa nyingine na kuhamia kwenye baa hiyo asubuhi akiendelea kunywa.

"Kulikuwa hakuna ugomvi wowote, huyu Alex aliyefanya tukio huwa ni mteja wangu, anakujaga ofisini kwangu na leo (jana) alikuja asubuhi akasema nimfungie 'seat cover' kwenye gari yake na tukafanya ile kazi kama kawaida, baada ya hapo akanikabidhi funguo ya gari na akaniambia nisiwe na wasiwasi atanipatia pesa yangu, akawa amekaa kwenye hii baa na wenzake ambao ninawafahamu," alisema shuhuda huyo.

"Baadaye wakati tumekaa kwenye meza nyingine tukiwa watu kama saba hivi kwenye hii baa, jamaa (Alex) akiwa katika sehemu yake aliyokaa na wenzake akawa anatoa bastola mara kwa mara, wenzake wakamwambia hicho anachokifanya siyo sahihi."

"Baada ya kumwambia hivyo, akaanza kuleta ubishi, lakini baadaye kidogo akajifikiria akaomba msamaha kwa wenzake na akatulia. Cha kushangaza baada ya kama dakila 10 hivi akanyanyuka tena kwenda chooni, kutoka kule akaja moja kwa moja kwenye meza yetu na kuanza kutoa maneno machafu."

"Hawa watu wanaojifanya watu wa usalama wako wapi." Alimnukuu na kuongeza.

"Akawa anatoa lugha chafu, akamwambia kwani umekuaje tena, akatoa silaha, wakati anakoki, risasi moja ikawa imedondoka nchini, akainama kuiokota. Mmoja wa waliofariki, anaitwa Gifti akamfuata kumwambia mbona unafanya hivyo."

Shuhuda huyo anaelezea kwamba wakati akifuatwa kuambiwa kwanini anafanya kitendo kile, tayari alimfyatulia risasi ya mguuni mwenzake aliyekuwa akimfuata kumtuliza kabla hajamfikia.

"Kabla Gifti hajamfikia kumtuliza asifanye kile alichokuwa anakifanya, alimfyatulia risasi ya kwanza ya mguuni, na nyingine tumboni, na wakati Gifti anakimbilia chooni, akamfuata tena na kumfyatulia ya kichwani akaanguka na kufa," alidai shuhuda huyo.

"Wakati Alex alipoanza kumshambulia Gifti, ilibidi sisi tukimbie na kujifungia ndani wakati huo tukiwa tunachungulia kuona anachokifanya, alibaki peke yake kwenye baa, akawa anaingia na kutoka nje huku akipiga risasi juu."

"Mara ya mwisho alipotoka nje na kurudi ndani kwenye baa, akamwangalia Gifti akiwa amelala chini ni kama alifahamu sasa kwamba tayari ameua, akasisimama akawa anaongea mwenyewe kwamba mnanijua mimi ni nani, mara akachukua silaha akijiwekea shingoni na kujipiga na akadondoka na kufariki papohapo."

Shuhuda mwingine anaelezea kwamba Alex hakuwa na ugomvi na mtu huyo aliyemuua isipokuwa ni ulevi ndio ulichangia afikie hatua hiyo.

"Hakukuwa na ugomvi wowote na hata yule kijana aliyeuliwa hawakuwa wanafahamiana, isipokuwa ni ulevi tu na walikutana hapo hapo baa," alidai shuhuda wa pili.

"Huyu jamaa aliyeua, alikuja hapa tangu asubuhi na inasemakana wakati anakuja hapa alikuwa ametoka kwenye baa nyingine na alikuwa amekesha huko anakunywa pombe, kwa hiyo alivyofika hapa alikuwa amelewa na tangu alipofika alikuwa ni kutishia watu."

Shuhuda wa tatu ambaye ni DJ kwenye baa hiyo ya Lemax, alisema mfanyabiashara huyo aliimuamrisha azime muziki.

"Huyu jamaa (Alex) alikuja kwangu akaniambia kwamba zima muziki, usalama tumefika, ikabidi nimwangalie, nikaona yuko 'serious' na akawa anaelekea kwenye meza waliokaa watu wengine, mara akafyatua risasi, Gifti akajaribu kumtuliza, yeye akampiga ya kwanza, mara akampiga ya pili, akawa ametawala baa yote, anaenda nje na kuingia ndani, watu wote wakakimbia."

"Baada ya kumpiga Gifti risasi ya tatu na kuona amedondoka chini, akatoka nje, akarudi tena ndani, dakika chache naye akajipiga risasi, akadondoka chini," anasimulia shuhuda wa tatu.

Kamanda wa Polisi Kinondoni, Ramadhani Kingai, alikiri kutokea kwa tukio hilo la mauaji saa 11:30 jioni juzi katika baa hiyo.

"Ni kweli tukio lilitokea saa 11:30 jioni na lilisababishwa na mfanyabiashara wa Kariakoo, Alex katika baa ya Lemix na sababu ya mauaji ni ulevi, inasemekana huyu mfanyabiashara alifika asubuhi ya saa nne na alitokea kwenye baa nyingine alikokuwa amekesha," alisema Kingai.

Miongoni mwa mambo yaliyoandikwa kwenye mitandao ya kijamii baada ya mfanyabiashara huyo kufanya tukio hilo ni kwamba Juni 13, mwaka huu alisherehekea siku yake ya kuzaliwa huku keki yake ikiwa imechorwa bastola.

"Alex, maarufu kama Simba, alisherehekea birthday yake Juni 13, 2021 na cake moja iliyokatwa siku hiyo ilikuwa na picha ya bastola na hii inaleta hisia kwamba huenda bastola ilikuwa kitu anachokipenda," ni miongoni mwa maneno yaliyoandikwa kwenye mitandao ya kijamii yakiambatanishwa na picha ya keki iliyoandikwa 'Happy Birthday Alex'.

# Wanaoshtakiana mashauri ya ardhi marufuku kulipia usafiri

**Na Munir Shemweta,** SONGWE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, amepiga marufuku wananchi wanaoshtakiana kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kugharamia usafiri wa kwenda uwandani wakati wa kusikiliza mashauri.

Akizungumza wakati wa kuzindua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Mkoa wa Songwe jana, Mabula alisema, asingependa kuona wananchi wanaoshtakiana katika kesi ya ardhi mmoja wao atoe fadhila ya usafiri wa kwenda uwandani.

"Tusingependa wale wanaoshtakiana mmoja wao atoe fadhila ya usafiri, maana baada ya hapo mara nyingi wazee wa Baraza wanashawishika na kuona anayetoa usafiri kuwa amekuwa ni msamaria mwema, kwa hiyo wanamlipa fadhila hata kama hana haki ya kupata ushindi," alisema Naibu Waziri Mabula.

Aliwataka Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi kuandaa ratiba za mashauri ya ardhi kwenye maeneo yao na kuzipeleka kwa wakuu wa wilaya aliowaeleza kuwa watashirikiana na wakurugenzi wa halmashauri kuangalia ratiba na kutoa usafiri kwa wazee wa mabaraza ili kwenda uwandani wakati wa mashauri.

Naye Kamishna wa Ardhi, Methew Nhonge, alisema pamoja na kuwa sheria ya ardhi imeainisha utaratibu mzuri wa kisheria katika kushughulikia migogoro ya ardhi, lakini halmashauri na ofisi za ardhi za mikoa zinao wajibu wa kuhakikisha migogoro ya ardhi kabla haijaenda mahakamani inatatuliwa kwa njia ya kiutawala.

"Bahati nzuri katika wizara tumeweka utaratibu kwa nchi nzima kuhakikisha kwamba viongozi wa ardhi wa mkoa pamoja na halmashauri kupitia watendaji wa sekta wanaenda kwenye ngazi za halmashauri na mitaa kutoa elimu na kushughulikia migogoro ya wananchi kiutawala," alisema Nhonge.

Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya nchini, Stela Tullo, aliushukuru uongozi wa mkoa wa Songwe kwa kusaidia kupata jengo la Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na kueleza kwamba, uanzishwaji baraza hilo utasaidia kuondoa usumbufu waliokuwa wakiupata wananchi wa Songwe kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za baraza mkoani Mbeya.

## HABARI KITAIFA

# CHADEMA yagoma kuwawekea dhamana viongozi wake

**Na Richard Makore,**
MWANZA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema hakina mpango wa kuwawekea dhamana viongozi wake waliokamatwa juzi na Jeshi la Polisi, jijini Mwanza.

Kimesema kwa sasa kinajiandaa na mkutano mwingine wa kudai Katiba mpya, baada ya polisi jijini humo kuvunja kikao chao na kuwakamata viongozi mbalimbali wa chama hicho mwishoni mwa wiki.

Juzi viongozi 38 wa chama hicho walikamatwa muda mfupi kabla ya kuanza mkutano wa kudai Katiba mpya na kushikiliwa katika vituo vya polisi vya Kirumba na Kati mkoani humo.

Akizungumzia sakata la kukamatwa viongozi hao jana, Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Vijana la chama hicho (BAVICHA), John Pambalu alisema, hawawezi kuwawekea dhamana kwa kuwa hawajui kosa la viongozi hao.

Pambalu alisema polisi wao wakitaka kukaa nao ni sawa na kama wakitaka kuwafikisha mahakama watajua wao, lakini chama hicho hakiwezi kwenda kuwadhamini.

Alisema kwa sasa wanachokifanya ni kuwapelekea chakula viongozi hao waliopo mahabusu za polisi.

"Viongozi hawa hawana kosa lolote, lakini kwa kuwa polisi wana hamu ya kukaa nao mahabusu wacha waendelee kufanya hivyo na kama wataamua kuwafikisha mahakamani pia watajua wao," alisema.

Pia, alisema kwa sasa kama BAVICHA wanaendelea na maandalizi ya kikao kingine cha kudai katiba mpya ambacho kitafanyika wiki hii jijini Mwanza.

Alisema Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe, anatarajia kushiriki katika mkutano huo.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema alitoa agizo juzi wanachama hao wa CHADEMA wapewe dhamana.

Wakati kamanda Ng'anzi akitoa kauli hiyo, Mwenyekiti wa BAVICHA, Pambalu alisema bado wanachama wao wanasota mahabusu mpaka jana jioni.

Jeshi la Polisi mkoani Mwanza juzi liliwashikilia watu 38 ambao miongoni ni viongozi wa BAVICHA, wafuasi wa chama hicho na kiongozi wa dini kwa madai ya kufanya mkutano wa kudai katiba mpya bila kibali.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kamanda wa Polisi mkoa huo, Ramadhani Ng'anzi, alisema miongoni mwa wanaowashikilia, wanawake ni sita.

Kamanda Ng'anzi alisema wengine wanaowashikilia ni Askofu Emmaus Mwamakula (Kanisa la Uamsho Moravian), ambaye aliliambia Jeshi la Polisi kuwa alikwenda katika mkutano huo kwa ajili ya kuuombea.

Aliwataja wengine wanaowashikilia kuwa ni Katibu Mwenezi wa Vijana Taifa, Mhadhiri mstaafu, Dk. Azaveli Lwaitama.

Kamanda Ng'anzi alisema CHADEMA walifanya matangazo mtaani kuujulisha umma kuwa juzi kutafanyika kongamano la kudai katiba mpya na kuwataka wananchi wahudhurie kwenye ukumbi waliopanga kufanya mkutano huo.

"Tuliwaandikia barua jana jioni (juzi) wasifanye mkutano baada ya gari la matangazo kupita mtaani, tuliwajulisha kwamba mkutano wa ndani hauna matangazo na walikuwa hawasemi wanachama bali wananchi wote waende kwenye kongamano," alisema.

Alisema bahati nzuri wengi walitii hawakuhudhuria kwa sababu waliona kosa lao, lakini wachache walikaidi ambao kwa sasa wanawashikilia watu 38.

"Tunawahoji kujua ni kwanini wanakusanyika baada ya kuwaambia wasikusanyike, endapo ushahidi utatosheleza kuna uwezekano wa kuwafikisha mahakamani kwa kufanya kusanyiko lisilokuwa halali," alisema.




Mbunge wa Masasi, Geoffrey Mwambe (kulia), akikabidhi mifuko ya saruji 100 aliyotoa katika kijiji cha Chipole, Kata ya Mumbuka Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa ajili ya kukarabati nyumba za walimu na kujenga matundu ya vyoo ya walimu katika Shule ya Msingi Chipole jana, mjini Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Shule 10,000 kukarabatiwa

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema serikali inatarajia kufanya ukarabati kwa shule zaidi ya 10,000.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana mjini Bagamoyo, mkoani Pwani katika makabidhiano ya vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Kaole, yaliyofanyiwa ukarabati na Taasisi ya Bilal Muslim kwa kushirikiana na Shirirka la Lady Fetma Trust la Uingereza.

Alisema kupitia tozo za miamala zinazokatwa kwa sasa kwenye simu zitasaidia kutatua kero za wananchi, ambapo kwa upande wa Wizara ya TAMISEMI miundombinu ya shule itakarabatiwa, lakini pamoja na zahanati na miundombinu ya barabara itaboreshwa.

"Tukifanikiwa kuanza ujenzi na ukarabati wa shule maana yake kwa miaka minne ijayo wanafunzi zaidi ya 450,000 kila mwaka watapata vyumba vya kusomea hakutakuwa na wanaosomea chini ya miti," alisema.

Alisema kuna shule za msingi zina watoto zaidi ya 800 na wengine wanakosa vyumba vya kukaa, hivyo ukarabati utakapoanza utasaidia kuondoa kero hiyo.

Aidha, Waziri Ummy alitoa maelekezo kwa wakurugenzi wote nchini kuhakikisha wanatenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutatua kero za wananchi ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya shule.

Alisema kipimo cha utendaji wa mkurugenzi itakuwa ni pamoja na anavyotenga fedha hizo, huku akisisitiza wenyeviti wa halmashauri kutoa kipaumbele cha utatuzi wa kero za wananchi upande wa elimu hususani maeneo ambayo yana uchakavu wa vyumba vya madarasa.

"Semina za kujadili elimu siyo kipaumbele, tutaangalia maendeleo ukarabati wa vyumba vya madarasa ndio vitu vya kuzingatia."

Aliwaomba wadau wa maendeleo kuendelea kusaidia kutatua kero za sekta ya elimu, ambapo alisema kwa sasa shule 7,000 ndiyo zilizochoka ambazo ukarabati wake unatarajia kuanza mwakani.

Mkurugenzi wa Bilal Muslim, Khairunbano Alinhai, alisema wamekuwa wakisaidia vitu mbalimbali kwa shule na ukarabati wa vyumba hivyo ambavyo vimegharimu Sh. milioni 70,000.

Alisema wataendelea kusaidia kwenye sekta ya elimu ili kuisaidia kuondoa kero zilizopo.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliishukuru taasisi hiyo, huku akieleza kuwa bado kuna upungufu wa vyumba vya madarasa katika mkoa huo.

# Watoto 981 wapata ujauzito kwa miezi 6

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO 981 katika Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, wamepatiwa ujauzito ndani ya kipindi cha miezi sita kilichoanzia mwezi Januari mwaka huu.

Kutokana na kitendo hicho cha ukatili wa kijinsia, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, ameagiza watuhumiwa watafutwe na kuchukuliwa hatua.

Naibu Waziri huyo alibaini hilo akiwa katika ziara ya siku tano wilayani humo iliyomalizika jana, iliyolenga kukagua na kujionea utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na masuala ya maendeleo ya jamii.

Katika ziara hiyo pia alizindua Kituo cha Huduma Jumuishi kwa waathirika wa vitendo vya ukatili wa Kijinsia (One Stop Centre) katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo kitakachowezesha walengwa kupata huduma kwa pamoja na kwa muda mfupi.

Alisema taarifa hizo haziwezi kufumbiwa macho, badala yake watendaji wanaohusika wafanye kila linalowezekana kuhakikisha watuhumiwa wanapatikana na haki inatendeka katika kipindi kifupi.

"Jamii haiwezi kutegemea miujiza ya mafanikio ya kizazi kijacho endapo itabaki kufumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani dhidi ya wanawake na watoto kwa kuangalia watoto wao wanapata mimba katika umri mdogo na kukatisha ndoto zao," alisema.

Alisema Sheria ya Mtoto inataja mashauri yao kukamilika ndani ya kipindi cha miezi sita, lakini kwa mazingira ya huduma za mkono kwa mkono, kuna umuhimu wa kuyamaliza muda mfupi zaidi.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DEEP CONSTRUCTION LIMITED** Inatangaza kupotelewa Kwa kadi yake ya gari aina yake **ISUZU FORWARD** yenye usajili namba **T 425 AJV CHASSIS NO.NNR12C3601987, ENGINE NO.6BG176819** Kwa yeyote atakaye ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **RB Na. MOR/MOR/ RB/311024/2021.**

11636802

**TANGAZO KUPOTEA HATI YA KIWANJA**

**Ramadhani Hassani Shemahonge** mkazi wa Bushushu Mwalugohe Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na Hati ya **Kiwanja Plot namba 97** Kitalu **RR (MD)** kilichopo eneo la **Bushushu Mwalugohe Manispaa ya Shinyanga.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo Karibu au awasiliane na Ramadhani Hassani Shemahonge kwa simu namba **0767436400.** **RB namba SHY/RB/ 2021/ Control namba 9910826245348.**

116364102

# Bei ya mbolea yaishtua serikali

**Na Enock Charles**

SERIKALI imeahidi kupunguza gharama za usafirishaji wa mbolea ili wakulima wapate mbolea hiyo kwa bei nafuu.

Hatua hiyo lengo lake ni kuachana na hali ya sasa ambapo gharama za pembejeo hizo ni ghari ikilinganishwa na miezi michache iliyopita.

Akizungumza na waagizaji na wasafirishaji wa mbolea mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wizara hiyo ina mpango wa kuzungumza na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kupunguza bei za usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka kwa wafanyabiashara kwenda maeneo mbalimbali.

"Tumekutana na waagizaji wa mbolea kujadili mambo mbalimbali, kwanza kujiridhisha tuna mbolea kiasi gani mwezi huu wa Julai na nani anaingiza kiasi gani mwezi huu wa Julai ili kusiwe na upungufu wa aina yoyote, " alisema Bashe.

"Mwezi Januari niliiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) kukaa na Shirika la Reli na leo nitakutana na Mkurugenzi Mkuu wa TRC ili kujadiliana suala la bei ya kusafirisha mbolea, pia upatikanaji wa mabehewa kwa wakati, " aliongeza.

Bashe alisema kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea kutoka katika soko la dunia kulikochangiwa na janga la corona, hali hiyo imesababisha kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo nchini, na hivyo kuwa mzigo kwa wakulima.

Akitolea mfano wa bei hizo Bashe alisema mbolea ya DAP awali ilikuwa ikiuzwa kwa Dola 416 za Marekani kwa tani 1, lakini sasa inauzwa kwa Dola takriban 650, UREA iliyokuwa ikiuzwa kwa Dola 359 sasa inauzwa kwa Dola 560, CAN iliyokuwa ikiuzwa kwa Dola 274 sasa inauzwa kwa Dola 420.

Kwa bei za mfuko mmoja Bashe alisema kwa mwezi Januari bei ya mbolea aina ya DAP ilikuwa Sh.71,000, lakini kwa sasa imefikia Sh. 100,000, pia mbolea aina ya UREA ilikuwa ikiuzwa kwa takriban Sh. 58,000, lakini sasa imefikia Sh. 87,000.

"Tumewaagiza vile vile TFRA na TARI kutoa elimu juu ya mbolea mbadala kupitia vipindi vya televisheni wakulima wasipate tabu ili kwa mfano wakikosa UREA wajue wanatumia mbolea gani kulingana na aina ya udongo alipo mkulima," alisema Bashe.

Katika hatua nyingine, Waziri Bashe alisema serikali itaendelea kuwekeza katika utafiti ili kuongeza ubora wa mbolea inayozalishwa ndani ili kujitosheleza katika mahitaji ya mbolea nchini kuliko kutegemea mbolea kutoka nje kila wakati.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza katika kongamano la Amani jana lililokuwa na dua maalumu ya kuombea viongozi na Taifa dhidi ya ugonjwa wa corona, ametoa wito kwa wananchi kulinda na kuitunza amani. **PICHA: JAMES LYATUU**

# Mambo 6 tozo miamala ya simu

**Na Waandishi Wetu**

SIKU chache baada ya utekelezaji wa bajeti ya serikali ya 2021/2022 kuanza na wananchi kulalamikia tozo za miamala ya simu, mambo sita yametajwa yatakayoleta mapinduzi katika tozo hizo.

Tozo hizo zimefafanuliwa kuleta faida kwenye uboreshaji wa barabara za vijijini, kuboresha shule za vijijini, hospitali za vijijini na kupeleka vifaa tiba.

Pia tozo hizo zimeelezwa kuwa zitaboresha mifumo ya maji vijijini, mifuko ya jimbo kuwezeshwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na kuboresha Mfuko wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

"Kwa mtu yeyote anayejua namna gani ya kukataa utegemezi katika kujenga nchi anakatwa anaumia, lakini anakuwa na tumaini kuwa kesho kinamama wajawazito hawatakufa njiani sababu ya barabara mbovu, wanafunzi watawahi shuleni, wafanyakazi watawahi maofisi na bidhaa za wakulima zitawahishwa minadani na katika viwanda."

Jana Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema ni lazima Watanzania sasa wafunge mkanda kwa ajili ya kutekeleza bajeti hiyo serikali kwa kuwa imekusudia kuongeza uwezo wa ndani wa kujitegemea kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika maeneo ya vijijini ambako ndiko kwenye uchumi mkubwa na idadi kubwa ya wananchi.

Profesa Kabudi, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo ya Katiba na Sheria uliofanyika mjini Morogoro na kuambatana na kutembelea miradi mikubwa ya serikali ambayo ni ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Rail) na Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere.

Alisema kuwa bajeti ya serikali imelenga kumkomboa mwananchi wa kijijini ili kuhakikisha anaweza kupata huduma bora kama kuwapo kwa miundombinu bora ya barabara ili kuweza kuhakikisha mazao yanazalishwa yanasafirishwa ili kwenda kuuzwa ndani na nje ya nchi ambako ndiko kwenye masoko ya uhakika.

Profesa Kabudi, alisema pia bajeti hiyo imelenga kuhakikisha kunakuwapo na huduma za umeme maeneo yote ya vijijini, ujenzi shule za uhakika pamoja huduma za afya na kwamba ili kuweza kufikia hayo ni lazima serikali ijenge uwezo wa kukusanya fedha za ndani katika vyanzo mbalimbali kutekeleza na sio kusubiri kusaidiwa au kupewa mkopo.

"Nchi yoyote ile ambayo inalenga kuleta mabadiliko ndani ya nchi yake ni lazima inatengeneza mazingira ya kuongeza kukusanya kupitia mapato yake ya ndani, sasa sisi tumeamua kuleta mabadiliko maeneo ya vijiji lazima tuongeze ukusanyaji wa mapato ya ndani na sio kusubiri kupewa mkopo au msaada," alisema Profesa Kabudi.

Akizungumzia kuhusu miradi mikubwa miwili ya ujenzi wa Bwawa la kufua Umeme la Julius Nyerere na Mradi wa Reli ya Kisasa, alisema serikali ilifanya uamuzi mzuri na wenye faida kwa taifa kwa kuwa utasaidia kuwapo kwa umeme wa uhakika na utachochea kuongezeka kwa viwanda pamoja na reli itakayosaidia kusafirisha mizigo mingi mpaka nchi za jirani.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kutembelea miradi hiyo miwili mikubwa ya kitaifa, nawasihi mkawe mashahidi na mabalozi wazuri juu yanayoendelea katika miradi hiyo huku mkiendelea kuinga mkono serikali ya awamu ya sita katika utekelezaji wake pamoja na mengine yote yanayoendelea ambayo mnayaona," alisema Waziri Profesa Kabudi.

Awali, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Sifuni Mchome, pamoja na kikao cha baraza hilo kujadili bajeti ya wizara hiyo, alisema wameona kutembelea miradi hiyo mikubwa miwili kwa kuwa wizara hiyo inahusika moja kwa moja katika sehemu ya utekelezaji wake.

Profesa Mchome, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo, alisema baraza hilo la wafanyakazi ni utekelezaji wa agizo namba moja la mwaka 1970 ukiwa na dhamira ya dhati ya kuwashirikisha watumishi kwenye mipango ya wizara kwa kuwa kila mtumishi anashiriki kwa uhuru na majadiliano ya ajenda zilizoainishwa.

**●Imeandaliwa na Ashton Balaigwa, Morogoro na Mwandishi Wetu, Dodoma**

# 10 kuanza kutoa ushahidi leo kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MASHAHIDI 10 wa upande wa Jamhuri wanatarajiwa kupanda kizimbani leo kutoa ushahidi wa mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha yanayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) na wenzake wawili, Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).

Pia vielelezo 10 vya ushahidi vinatarajiwa kuwasilishwa mahakamani katika kesi hiyo ya jinai namba 105 ya mwaka 2021.

Julai 16, mwaka huu, akizungumza mahakamani wakati washtakiwa hao wakisomewa maelezo ya awali ya mashtaka yanayowakabili na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tumaini Kweka, alidai kwamba upande Jamhuri una mashahidi wasiopungua 10 au kuzidi idadi hiyo pamoja na vielelezo vya ushahidi visivyozidi au kupungua 10. "Mheshimiwa Hakimu bila ya kupoteza muda napenda kuieleza mahakama yako kwamba upande wa Jamhuri sisi tuna mashahidi wasiozidi au kupungua 10, pamoja na vielelezo vya ushahidi usiopungua au kuzidi 10," alidai wakili huyo wa serikali, Tumain Kweka.

Katika hatua nyingine, upande wa Jamhuri uliondoa mahakamani mashtaka mawili ya awali ya unyang'anyi wa kutumia silaha yaliyokuwa yakiwakabili washtakiwa hao, katika kesi ya jinai namba 66 ya mwaka 2021.

Washtakiwa hao waliachiwa huru na walikamatwa tena na kusomewa mashtaka mengine mapya matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kusomewa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya mashtaka kwa washtakiwa hao, Wakili Abdallah Chavula, alidai shtaka la kwanza ni la unyang'anyi wa kutumia silaha linalowakabili washtakiwa hao. Alidai mshtakiwa wa kwanza Ole Sabaya (34), Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), Februari 9, mwaka huu, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. milioni 2.769, mali ya Mohamed Saad, na baada ya kufanya wizi huo walitumia silaha ya bunduki kuwatisha waliokuwa kwenye duka hilo.

Shtaka la pili, ni unyang'anyi wa kutumia silaha, ikidaiwa wote kwa pamoja, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba kiasi cha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi, na baada ya wizi huo walimfunga na pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake. Katika shtaka la tatu la wizi wa kutumia silaha, ilidaiwa mahakamani, Ole Sabaya na wenzake, Februari 9, mwaka huu, Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja na fedha Sh. 35,000 mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wapatiwe fedha na mali walizoiba.

# TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# SONGWE DISTRIC COUNCIL

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SONGWE DISTRICT COUNCIL

STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 20 | 2,384,864,973 | 2,956,932,547 |
| Receivables and prepayments | 21 | 976,597,388 | 736,885,269 |
| Inventories | 22 | 572,170,286 | 310,206,245 |
| | | 3,933,632,647 | 4,004,024,061 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other Finance Assets | 23 | 16,000,000 | 11,000,000 |
| Property, plant and equipment | 28 | 21,038,636,268 | 21,059,092,587 |
| | | 21,054,636,268 | 21,070,092,587 |
| **TOTAL ASSETS** | | 24,988,268,915 | 25,074,116,648 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 24 | 1,662,096,016 | 1,406,353,433 |
| Deferred income (Grant) | 11 | 347,131,809 | 264,147,449 |
| | | 2,009,227,825 | 1,670,500,883 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income (Grant) | 27 | 1,682,414,754 | 2,226,318,694 |
| | | 1,682,414,754 | 2,226,318,694 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 3,691,642,578 | 3,896,819,577 |
| **NET ASSETS** | | 21,296,626,336 | 21,177,297,070 |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 21,260,626,336 | 21,141,297,070 |
| Minimum Compulsory Reserve | | 36,000,000 | 36,000,000 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | 21,296,626,336 | 21,177,297,070 |

The financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 24th September, 2020 and were signed on its behalf by:

Fauzia Hamidu Ngatumbura
CMT Chairperson
Date: 24/09/2020

William Mwakalambile
CMT Secretary
Date: 24.09.2020

MKURUGENZI MTENDAJI (W) SONGWE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SONGWE DISTRICT COUNCIL

STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 1,804,734,301 | 1,621,234,541 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 698,051,832 | 484,574,154 |
| Amortisation of revenue grants | 11 | 10,171,692,780 | 9,309,179,696 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 10,005,037 | 1,850,400 |
| Revenue from non-exchange transactions | 13 | 106,565,227 | - |
| Other revenue | 14 | 308,548,309 | 273,580,893 |
| Amortisation of capital grant (Rev. non exchange transactions) | 27 | 2,175,577,317 | 3,368,174,310 |
| | | 15,275,174,802 | 15,058,593,993 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 15 | 10,032,813,937 | 8,250,304,953 |
| Supplies and consumables used | 16 | 1,403,185,928 | 769,177,236 |
| Maintenance expenses | 17 | 791,768,240 | 507,844,573 |
| Grants and other transfer payments | 18 | 234,442,132 | 1,792,707,274 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 28 | 508,101,072 | 770,756,163 |
| | | 12,970,311,309 | 12,090,790,198 |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 2,304,863,493 | 2,967,803,795 |
| **Attributable to:** | | | |
| Owners | | 2,304,863,493 | 2,967,803,795 |
| | | 2,304,863,493 | 2,967,803,795 |

The financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 24th September, 2020 and were signed on its behalf by:

Fauzia Hamidu Ngatumbura
CMT Chairperson
Date: 24/09/2020

William Mwakalambile
CMT Secretary
Date: 24.09.2020

MKURUGENZI MTENDAJI (W) SONGWE

## 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Songwe District Council,
P.O. Box 77,
**MKWAJUNI - SONGWE.**

## 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

### Opinion

I have audited the Financial Statements of Songwe District Council which comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2020, and the Statement of Financial Performance, the Statement of Changes in Net Assets and Cash Flow Statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of the Songwe District Council as at 30th June, 2020, and its Financial Performance and Cash Flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act 1982 (Revised 2000).

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Songwe District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

### Key Audit Matters

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

### Other Information

Management is responsible for the other information. The other information comprises the Councilor's Report and the Declaration by the Head of Finance but does not include the financial statements and my audit report thereon.

### Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements

My objectives are to obtain reasonable assurance about whether the financial statements as a whole are free from material misstatement, whether due to fraud or error, and to issue an audit report that includes my opinion. Reasonable assurance is a high level of assurance but is not a guarantee that an audit conducted in accordance with ISSAIs will always detect a material misstatement when it exists. Misstatements can arise from fraud or error and are considered material if, individually or in the aggregate, they could reasonably be expected to influence the economic decisions of users taken on the basis of these financial statements.

As part of an audit and in accordance with ISSAIs, I exercise professional judgment and maintain professional skepticism throughout the audit. I also:

- Identify and assess the risks of material misstatement of the financial statements, whether due to fraud or error, design and perform audit procedures responsive to those risks, and obtain audit evidence that is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion. The risk of not detecting a material misstatement resulting from fraud is higher than for one resulting from error, as fraud may involve collusion, forgery, intentional omissions, misrepresentations, or the override of internal control;
- Obtain an understanding of internal control relevant to the audit in order to design audit procedures that are appropriate in the circumstances, but not for the purpose of expressing an opinion on the effectiveness of the entity's internal control;
- Evaluate the appropriateness of accounting policies used and the reasonableness of accounting estimates and related disclosures made by management;
- Conclude on the appropriateness of management's use of the going concern basis of accounting and, based on the audit evidence obtained, whether a material uncertainty exists related to events or conditions that may cast significant doubt on the entity's ability to continue as a going concern. If I conclude that a material uncertainty exists, I am required to draw attention in my audit report to the related disclosures in the financial statements or, if such disclosures are inadequate, to modify my opinion. My conclusions are based on the audit evidence obtained up to the date of my audit report. However, future events or conditions may cause the entity to cease to continue as a going concern; and
- Evaluate the overall presentation, structure and content of the financial statements, including the disclosures, and whether the financial statements represent the underlying transactions and events in a manner that achieves fair presentation.

I communicate with those charged with governance regarding, among other matters, the planned scope and timing of the audit and significant audit findings, including any significant deficiencies in internal control that I identify during my audit.

I also provide those charged with governance with a statement that I have complied with relevant ethical requirements regarding independence, and communicate with them all relationships and other matters that may reasonably be thought to bear on my independence, and where applicable, related safeguards.

From the matters communicated with those charged with governance, I determine those matters that were of most significance in the audit of the financial statements of the current period and are therefore the key audit matters. I describe these matters in my audit report unless law or regulation precludes public disclosure about the matter or when, in extremely rare circumstances, I determine that a matter should not be communicated in my report because the adverse consequences of doing so would reasonably be expected to outweigh the public interest of such communication.

In addition, Section 10 (2) of the Public Audit Act, 2008 requires me to satisfy myself that, the accounts have been prepared in accordance with the appropriate accounting standards.

Further, Section 48 (3) of the Public Procurement Act, 2011 requires me to state in my annual audit report whether or not the audited entity has complied with the procedures prescribed in the Procurement Act and its Regulations.

## 1.2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011 (as amended in 2016)**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**
I performed compliance audit on procurement of works, goods and services of Songwe District Council for the financial year 2019/20 as per stipulations of Public Procurement Act, 2011 and its Regulations of 2013 (as amended in 2016).

**Conclusion**
Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, procurement of goods, works and services of Songwe District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Act, 2011 and its underlying Regulations of 2013 (as amended in 2016).

1. **Procurement made without Tender Board approval TZS 160,000,168**
   Reg. 55 (2) of PPR, 2013 (as amended in 2016) requires the Procurement Management Unit (PMU) before inviting tenders, to furnish to the Tender to Board for its approval the text of the invitations to tender and the specifications or the expression of interest and terms of reference, other tender or proposal and draft contract documents together with a description of the advertising procedure to be followed for the tender or proposal, and shall make such modifications in the said documents or procedures as the tender board shall direct. Contrary to the above, during the audit I noted that, Songwe District Council procured building materials from different suppliers for construction of Council administration block worth TZS 160,000,168 without obtaining Tender Board approval.

2. **Procurement made without competitive quotations TZS 132,357,977**
   During the audit I noted procurement of building materials worth TZS 132,357,977 which were not supported with competitive quotations contrary to Reg. 164 (1) of PPR, 2013 (as amended in 2016) which requires quotations to be obtained from at least three suppliers.

3. **Delivery of procured building materials without inspection by an Inspection and Acceptance Committee TZS 369,013,533**
   The Council management received and accepted building materials worth TZS 369,013,533 without being inspected contrary to Reg. 244 (1) of PPR, 2013 (as amended in 2016) which requires goods delivered to be inspected, sampled and tested by the procuring entity before being accepted.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**31st March, 2021**

216364002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji, timu zijipange kwa usajili

**LIGI** Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2020/21 imefikia tamati jana, kwa mabingwa Simba kukabidhiwa kombe lao ikiwa imelitwaa kwa mara ya nne mfululizo.

Simba ilikabidhiwa taji hilo baada ya mchezo wake dhidi ya Namungo FC mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kumalizika kwa ligi hiyo maana yake sasa ni maandalizi kwa ajili ya msimu mpya wa 2021/22.

Timu sasa zinafanya tathmini ya kile ilichovuna kuanzia mwanzo wa mashindano hadi mwisho, kama wamefikia malengo au wamekwama.

Ikiwa wamefikia malengo ni jambo zuri, lakini kama wamefeli waangalie wapi walipojikwaa na kurekebisha baadhi ya makosa waliyofanya ili yasijirudie katika msimu ujao wa ligi.

Kumalizika kwa ligi hiyo sasa timu zimeanza kuimarisha vikosi vyao kama kufanya sajili za wachezaji wapya ili tu kuimarisha mabenchi yao ya ufundi kwa ajili ya msimu unaokuja wa Ligi Kuu ya Tanzania.

Licha ya kuwa dirisha la usajili bado halijafunguliwa, tayati timu zimeanza kuangalia na kuwataja wachezaji ambao wanawania kuwasajili ili kuimarisha vikosi vyao.

Katika madirisha ya usajili mara nyingi kumekuwa na utata hasa kwa wachezaji kusaini timu zaidi ya moja, tuliwahi kuona kwa nyota kama winga Mrisho Ngasa mwaka 2013 wakati akijua fika ana mkataba na Azam FC, lakini alisaini mkataba wa siri na Yanga jambo lililomfanya apigwe faini ya Sh. milioni 45 kwa kosa hilo.

Kiungo mshambuliaji Mohamed Mkopi mwaka 2016 alijikuta akikaa nje ya uwanja mwaka mzima baada ya kusaini timu mbili wakati akijua fika bado hajamalizana na waajiri wake Tanzania Prisons, akasaini kwa watani wao wa jadi Mbeya City jambo lililomfanya akutane na rungu hilo.

Pius Buswita, ambaye alidumu katika kikosi cha Yanga kwa miaka miwili wakati anaondoka Mbao aliingia kandarasi na Simba lakini baadaye akasaini Yanga, jambo ambalo likamfanya apitiwe na rungu la kufungiwa na kutakiwa kurudisha fedha za Simba.

Naye kiungo wa zamani wa Kagera Sugar, Ludovic Venance mwaka 2017 alipitiwa na rungu baada ya kusaini mkataba mpya na African Lyon, wakati akijua fika kuwa bado ni mwajiriwa wa Mbao FC, ambapo alijikuta akikosa michezo minne ya timu yake mpya.

Sakata kama hili pia limetokea msimu wa 2020/21 ambapo kiungo Benard Morrison, amesaini kandarasi na Simba wakati klabu ya Yanga ikidai kuwa ina mkataba na mchezaji huyo ambapo hadi sasa kesi ya wawili inaendelea katika mahakama ya usuluhishi CAS.

Wakati tukisubiri Shirikisho la Mpira wa Miguu kutangaza tarehe ya ufunguzi wa dirisha la usajili nataka kutoa rai kwa wachezaji pamoja na klabu kuwa makini kipindi hiki ili kukwepa kukutana na adhabu za kufungiwa na kulipishwa faini kwa kosa ambalo limekuwa likijirudia misimu nenda rudi.

Nipashe tunaamini timu pamoja na wachezaji watajifunza kupitia kwa mifano hii ambayo iko wazi ili kulinda taswira ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na wao katika jamii ya wapenda soka.

Kwa sababu mchezo wa soka ni wa burudani hivyo, haipendezi kuona wachezaji wakifungiwa kwa kutokuwa makini kwenye usajili, hivyo tunaamini kwamba, sakala hilo halitatokea kuelekea kwenye dirisha la usajili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Maandalizi Ligi Kuu 2021/22 yaanze sasa

**LIGI** KUU Tanzania msimu wa 2020/21 ilimalizika jana ili kuwapa nafasi wachezaji, makocha kwenda makwao kupumzika kwa muda kabla ya kuanza kwa msimu mwingine mpya wa 2021/22.

Ligi hiyo imemalizika huku kila timu ikivuna ilichopanda kwa msimu mzima.

Kwanza kabisa niipongeze Simba kwa kutwaa ubingwa wa msimu huu ambao unakuwa ni wa nne mfululizo.

Niipongeze pia timu ya Yanga kwa kumaliza kwenye nafasi ya pili ambayo imeifanya kukata tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

Imepata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, lakini kama itatwaa Kombe la FA kwa kuifunga Simba mjini Kigoma Julai 25, inaweza kuamua kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Hilo lilikuwa linazungumzwa sana na baadhi ya viongozi wa Yanga ambao wanaonekana hawataki mbeleko ya Simba kwenye mechi za kimataifa.

Wao wadai wataka wacheze michuano ya kimataifa kwa nguvu zao wenyewe na si kwa mgongo wa mtu.

Kufanya vema kwa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kumechangia Tanzania kupata pointi ambazo zimeifanya kuongezewa timu za kushiriki kutoka mbili hadi nne.

Pongezi zingine zinakwenda kwa Azam FC. Nayo inarejea tena kwenye michuano ya kimataifa baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu uliopita.

Itacheza Kombe la Shirikisho kwa sababu ya kushika nafasi ya tatu, lakini kama Yanga ikitwaa Kombe la FA na kuamua kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, basi itakwenda kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania, timu kutoka mkoani Mara, Biashara United itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho baada ya kukamata nafasi ya nne.

Nitoe pongezi kwa viongozi, wachezaji, makocha na mashabiki wa timu hiyo kwa kutimiza ndoto hiyo, kwani kuna timu zipo muda mrefu kwenye Ligi Kuu, lakini zimeshindwa kupata nafasi hiyo.

Baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, ni wakati sasa wa viongozi wa klabu hizo kukaa na kutafakri nini kilifanyika, wapi walikosea, wapi walifanya vema. Na ni kipi wafanye kwa msimu ujao wa ligi.

Wakati wachezaji na makocha wanakwenda kupumzika, huu si wakati wa viongozi kupumzika.

Naweza kusema kuwa huu ndiyo wakati wa viongozi wa klabu kufanya kazi zaidi kuliko wakati ligi inachezwa.

Ni wakati kwanza wa kuzifanyia kazi ripoti za makocha ambazo wamezitoa baada ya ligi kumalizika.

Makocha watakuwa wamekabidhi ripoti zao kuonyesha sehemu ambazo zina mapungufu na kuzifanyia kazi.

Kutokana na Ligi ya Tanzania kuchelewa kumalizika muda uliobaki ni mchache tu kabla ya kuanza kwa michuano ya kimataifa.

Nimeona tayari klabu ya Azam imeshaanza kufanya usajili. Hili ndilo linatakiwa. Ni wakati wa kufanya usajili haraka ili wachezaji wanaokuja wapate muunganiko wa wenzao mapema, badala ya kusubiri dakika za mwisho, halafu wanakuja wachezaji ambao wanaombewa muda na viongozi ili wazoeane na wenzao, wakati walitakiwa wasajiliwe mapema.

Kwa upande wa timu ambazo zitasubiri Ligi Kuu, viongozi wanatakiwa kwanza wajue nani anaondoka, nani anabaki. Mchezaji gani anaondoka kwa kumaliza mkataba na yupi ambaye wanamuuza.

Kipindi hiki ndicho ambacho klabu zinatakiwa kuwa na pesa ya kusajili wachezaji na si ligi inataka kuanza ndipo viongozi wanaanza kupitisha bakuli kwa wadau eti kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya.

Naweza kusema kuwa hiki ndicho kipindi kigumu zaidi kwa viongozi wa klabu za soka na inabidi kukitumia vizuri, kwani kunaweza kuifanya timu ikawa bora na yenye kuleta ushindani au bora timu.

Msingi wa timu bora inaanza kwa kusajili wachezaji mapema. Haiwezekani ligi inataka kuanza ndiyo viongozi wanaanza kukimbizana na muda kwenye usajili.

Ikumbukwe kuwa msimu ujao kutakuwa na timu 16 tu, hivyo viongozi wanatakiwa kusajili wachezaji bora na kutengeneza timu yenye ushindani na hilo haliwezekani kama maandalizi hayatofanyika mapema.

Huu ndiyo wakati muafaka wa kufanya hivyo. Wakati Ligi Kuu msimu huu umemalizika, ndiyo maandalizi ya msimu mwingine uanze sasa. Kuchelewa kufanya hivyo kwa sababu yoyote ile, iwe kutegeana, kutokuwa na pesa za usajili, kutojua wachezaji wa kuwasajili, au kusubiri wachezaji wenye viwango vidogo, ni kujichimbia kaburi kwa msimu ujao.

Mashabiki wamechoka na misemo ya "tuwape muda" au "muunganiko bado."

HABARI KITAIFA

# RITA yasajili vyeti kuzaliwa 10,495

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umevunja rekodi ya kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi 10,495 ndani ya siku 16 katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba).

Akitoa taarifa hiyo kutoka katika banda la RITA viwanja vya Sabasaba, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Emmy Hudson, amesema kuwa wananchi wamekuwa na mwitikio mkubwa wa kufuatilia vyeti vya kuzaliwa kutokana na kujua umuhimu wa kuwa na cheti hicho ili kujipatia mahitaji muhimu katika jamii.

Hudson alisema mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na wananchi waliofika katika banda hilo kwa ajili ya kupata vyeti vya kuzaliwa siku ya kufungwa kwa maonyesho hayo.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa RITA kuwafikia wananchi katika kila sehemu na kutoa huduma pamoja na kwenye maadhimisho na maonyesho mbalimbali kama hayo ili kuwarahisishia upatikanaji wake karibu na maeneo wanayoishi.

Alisema licha ya maonyesho hayo kumalizika, wataendelea kutoa huduma hiyo katika ofisi za RITA kama kawaida na wananchi wanatakiwa kuendelea kufika ili kupata vyeti kwa kuwa ni haki ya kila Mtanzania.

"Changamoto tuliyoipata Uwanja wa Sabasaba ni watu kuwa wengi, ambapo ikasababisha huduma hiyo kutolewa hadi saa moja usiku, ili kila aliyefika katika banda hili aweze kupata huduma kulingana na mahitaji yake," alisema Hudson.

Mmoja wa wananchi hao, Amina Abdallah, aliipongeza RITA kwa huduma hiyo na yeye kufanikiwa kupata cheti chake cha kuzaliwa kwa gharama nafuu na kwa haraka.

"Kwakweli wananchi tulikuwa wengi sana ambao tunahitaji huduma ya vyeti, lakini tulipokelewa vizuri na maofisa wa RITA waliokuwa wanatoa huduma na kutuhudumia kulingana na mahitaji yetu," alisema.

Joseph Mashaka alisema, hakuwahi kutegemea kupata cheti cha kuzaliwa kulingana na umri wake kutokana na baadhi ya wananchi mtaani kutoa taarifa za upotoshaji kuhusu ugumu wa kupata huduma hiyo, lakini baada ya kufika katika banda hilo alipewa maelekezo na kisha kuanza hatua za kupata cheti tofauti na alivyodhani hapo awali.

Mmoja wa viongozi waliotembelea banda hilo ni Meya wa Jiji la Ilala, Omary Kumbilamoto, ambaye aliupongeza wakala kwa kutoa huduma hiyo hadi muda wa usiku kwa lengo la kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya cheti cha kuzaliwa.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ali Hapi, akizungumza kwenye hafla ya makabidhiano iliyofanyika katika Shule ya Msingi Buhare, NMB imetoa mabati 750, madawati 157 kwa ajili ya shule za mkoa wa Mara na vitanda 8 vya kujifungulia kwa ajili ya Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Fedha, Juma Kimori na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Alfany Haule. Benki ya NMB imekabidhi vifaa vikiwa na thamani zaidi ya Shilingi milioni 68 mkoani Mara, ikiwa ni sehemu uwajibikaji wake kwa jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waathirika Kariakoo walilia mikopo ya riba nafuu

**Na Christina Mwakangale**

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu la Kariakoo walioathiriwa baada ya soko kuungua, wameiomba serikali na wadau zikiwamo taasisi za kifedha, kuwapatia mikopo yenye riba nafuu na ya muda mrefu, ili wanunue bidhaa na kurejea katika shughuli zao kama awali.

Katibu wa Vigoli vya Mzunguko wa Biashara Sokoni Kariakoo, Anna Mzena, akizungumza na Nipashe jana, ikiwa ni wiki moja baada ya tukio la moto, alisema tatizo lilipo ni mtaji pamoja na serikali kuwa nao karibu na kuwapa ushirikiano, ikiwamo kuwagawia maeneo ya biashara Kisutu na Machinga Complex.

Alisema akiwa kiongozi wa wafanyabiashara hao wapatao 124 walioungaliwa mali zao ni 99 na waliobaki 19, hawakuathirika kama wenzao.

"Naongoza wafanyabiashara katika umoja wetu wapatao 124, kati yao 99 wameathirika na moto, waliobaki wako salama. Na hivi karibuni walioathirika na moto huo nimewajazia fomu za kuonyesha walivyoathirika," alisema Anna.

"Tumepata hifadhi Kisutu, ingawa nafasi ni ndogo haitoshelezi, na serikali wana msaada mkubwa kama kutoka kwa DC (mkuu wa wilaya) na RC(mkuu wa mkoa) pamoja na ofisa biashara Mkoa na Jiji. Wakati kesho (leo) tukisubiri kauli ya Waziri Mkuu, tusubiri, ila hatujui hatima yetu."

Anna alibainisha kwamba wafanyabiashara hao walio wengi ni watu wazima wenye majukumu ya kifamilia, hivyo kuanzisha shughuli nyingine ni kikwazo kwao, na kwamba mikopo nafuu itawarudisha sokoni kutafuta riziki.

"Tukopeshwe kwa riba nafuu na mkopo wa muda mrefu, sababu watu wameathirika kisaikolojia, wengine maradhi yameanza, ili turudi barabarani, wengi umri umeenda utaanza shughuli gani mpya," alisema Anna.

Makamu Mwenyekiti Machinga Taifa Stephen Lusinde, aliiambia Nipashe kwamba, pamoja na walioathiriwa kupunguza matatizo yao kwa baadhi kupata maeneo mapya, bado kuna suala la ufinyu wa maeneo na mtaji.

Alisema kati ya wafanyabiashara 1,636 walioathiriwa na moto waliopata maeneo mapya ya biashara ni 570 baadhi katika mtaa wa Swahili na wengine kupelekwa soko la Kisutu na Machinga Complex.

"Mtaa wa Swahili hapa Kariakoo ni maalumu wamepatiwa wafanyabiashara hawa na kati ya 570 waliopo mtaa huu ni zaidi ya 340, na waliokuwa wanauza mazao sokoni wameenda Machinga Complex," alisema Lusinde.

"Machinga Complex tumepata wafanyabiashara wengine waliobaki na patatosha, ila kuanza sehemu eneo jipya umeunguliwa, hivyo tunawaelimisha waanze biashara walikopangiwa sababu kilichotokea hakikupangwa, wakubaliane na hali."

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Soko Kuu Kariakoo, John Shao, alisema wafanyabiashara hao wamepata maeneo kuanzia juzi ingawa ni nafasi chache.

"Nafasi ni chache mfano, aliyekuwa na maduka matatu, manne atapata sehemu moja, watu wa nyama na samaki, dawa, walipata soko la Kisutu na wanaouza machuma wapo Machinga Complex," alisema Shao.

# TRA yajikita kuchochea ulipaji kodi kwa hiari

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema kwa sasa ipo katika hatua ya kuboresha zaidi utendaji wa shughuli zake, ikiwamo kukuza mfumo wa kisasa wa usimamizi wa kodi ili kuchochea uhiari kwa walipakodi.

Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka hiyo, Alphayo Kidata, hatua hiyo itasaidia kuimarisha zaidi utendaji wa mamlaka hiyo, ukusanyaji wa mapato kwa vipindi vya kati na vya muda mrefu, kuongeza mapato ya ndani na pia kuchangia maendeleo ya biashara nchini.

Kidata alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la siku tatu la wataalamu kutoka Bodi ya Kitaifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na TRA lililolenga kujadili masuala ya bajeti, uchumi na ukusanyaji wa mapato.

"Kwa nchi yetu kufikia malengo kadhaa ya maendeleo ambayo tumejiwekea ikiwa ni pamoja na kukuza uchumi wa viwanda, kuwa na mfumo thabiti na endelevu wa ukusanyaji mapato hakuepukiki. Mfumo endelevu wa ukusanyaji mapato ambao tunahitaji katika nchi yetu ndio utatuonyesha dira na utachochea imani kwa siku zijazo kwa kuruhusu ukuaji wa biashara badala ya kuzididimiza," alisema Kidata.

Alisema kiu ya serikali ya awamu ya sita ni kuona walipakodi na wafanyabiashara sio tu wanaimarika,bali pia kuhakikisha wanazingatia sheria na kanuni za ulipaji kodi zilizopo.

"Ndio maana TRA inajitahidi kulinda uhusiano mzuri na ushirikiano wa kibiashara kati yake na walipa kodi, na siyo kujenga chuki," alisema Kidata.

# Moto wateketeza nyumba, Zimamoto ikilaumiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MOTO umeteketeza nyumba moja inayomilikiwa na Mzee Abdul maarufu kwa jina la 'Baba Tabu' iliyopo Mtaa wa Airport jijini Dodoma, huku wananchi wakilalamikia Jeshi la Zimamoto kushindwa kuuzima kwa wakati kutokana na kufika na gari bila maji ya kutosha.

Hata hivyo, pamoja na wananchi kusaidia kuzima moto huo kwa kutumia ndoo za maji, jitihada zao hazikuzaa matunda kutokana na kasi kubwa ya moto.

Tukio hilo lilitokea juzi saa nne usiku ambapo mmoja wa mashuhuda aliyejitambulisha kwa jina la Mnyami, alisema moto huo ulianza kidogo upande wa duka la majeneza, lakini simu ilipigwa mapema kwa Zimamoto ambao walifika na gari likiwa na maji kidogo.

"Kama muda waliofika Zimamoto wangekuwa na maji, moto ungedhibitiwa, tunashauri wanapopigiwa simu waje na gari mbili zenye maji, maana wanapofika na kukuta moto halafu wanaondoka kwenda kufuata maji wanasababisha moto kuteketeza vitu, huo muda wa kuchukua maji na kurudi nyumba inakuwa imeteketea," alisema.

Naye Mariam Mbaruku alisema uzembe wa jeshi hilo ni moja ya sababu zilizochangia nyumba hiyo kushika moto kwa kasi kwa kuwa walifika wakati ukiwa na kasi ndogo, lakini waliondoka kudai wanafuata maji.

"Nyumba ya baba Tabu imeteketea na nyumba ya pili ilianza kushika moto, nimeumia sana nyumba ya huyu baba ni mzee sana na ndio anayoishi na watoto wake. Hivi karibuni tumemzika mke wake na mtoto, na yeye ni mgonjwa kama jirani nimeumia sana," akisema na kuongeza:

"Hawa Fire hawana umakini, hii nyumba inatazamana na uwanja wa ndege, hivi kweli gari lililopo uwanja wa ndege lilikuwa halioni huu moto?"

Diwani wa Kata ya Viwandani, Jafari Mwanyemba, alisema saa nne alipata habari kuwa kuna moto na kutoa taarifa kwa jeshi hilo, na kwamba baada ya gari la kwanza kutoka Makao Makuu ya Zimamoto kufika likiwa na maji kidogo na kulazimika kwenda uwanja wa ndege kuomba gari ambalo lilifika likiwa na maji ya kutosha na kuzima moto huo licha ya kuwa tayari ulikuwa umeteketeza mali zilizokuwapo.

"Wananchi wengi hawajui kuwa gari la Fire sio muda wote linakuwa limejaa maji, bali hubaki na maji kidogo kwa ajili ya dharura, nadhani kule wanapochukua maji pia huenda walikuta kasi ya maji ni ndogo, nyumba ya Mzee Abdu kwa kweli imeteketea na kuna chumba kimoja cha gesti ya pili hapa kilidaka moto, lakini wamewahi, hali si nzuri kwa kweli," alisema.

Aidha, alisema bidhaa za kwenye maduka ya nyumba hiyo ikiwamo matairi zimechangia kuchochea moto huo.

"Hizi nyumba ambazo tunatengeneza na vyumba vya biashara tuchukue tahadhari tuache nafasi kati ya nyumba kwa nyumba, kwa mfano hapa mtaa mzima ungeungua kwa kuwa eneo lote linatumika kwa biashara, na tuache nafasi kwa ajili ya dharura kama hizi za moto," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ramadhan Kailima, alisema jeshi hilo litafanya tathmini ya athari na chanzo cha moto baadaye.

"Naomba wananchi wawe wavumilivu miundombinu yetu ya upatikanaji wa maji bado haijawa rafiki, hatutoi maji mbali lakini moto ukiwaka gari kutoka Makao Makuu pale ya Zimamoto hadi ifike hapa kuzima ni hasara, magari yapo imara ingawa tungekuwa na kisima cha maji eneo hili tungefunga mpira ili kuzima moto," alisema.

Kailima alisema duniani kote gari la zimamoto hufika na maji ya dharura na wanapomaliza hufunga kwenye kisima mpira ili kuendelea kukabiliana na moto.



Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Vodacom, Jacquiline Materu, akikabidhi choo kwa ajili ya kujistiri kwa wanafunzi wa kike. Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation imejenga na kukabidhi choo kipya katika Shule ya Msingi Mango iliyoko wilayani Kibosho mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hukumu dhidi Mhadhiri UDSM matunzo ya watoto, Julai 29

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Watoto Kisutu inatarajia kutoa hukumu dhidi ya Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Aviti Mushi na Getrude Mushi, wanaobishana matunzo ya watoto, Julai 29, mwaka huu.

Uamuzi huo wa mahakama umefikiwa baada ya Hakimu Devotha Msofe, kusikiliza malalamiko ya Getrude na majibu ya Dk. Aviti.

Mlalamikaji katika shauri hilo anadai wamefanikiwa kuzaa watoto wawili na mlalamikiwa ambao wanahitaji kupata matunzo kutoka kwa baba huyo.

Anadai kwa sasa watoto wako chini ya uhifadhi wa mama na mlalamikiwa anawajibika kutunza watoto wake, lakini tangu 2020 hajatoa matunzo ya aina yoyote ikiwamo ada.

Getrude anadai alipeleka taarifa Ustawi wa Jamii Mei, mwaka jana na Desemba 11 mwaka huo alikubali kutoa matunzo, lakini hakutekeleza.

Mlalamikaji anadai katika makubaliano alikubali kulipa ada za shule na atatoa Sh. 700,000 kwa mwezi.

Baada ya mlalamikiwa kukiuka makubaliano shauri hilo lilifikishwa mahakamani Juni 9, mwaka huu kwa faida ya watoto na limesikilizwa na kupangwa kwa ajili ya hukumu Julai 29, mwaka huu.

# Vijiji 20 havina umeme Ludewa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Jimbo la Ludewa mkoani Njombe, Joseph Kamonga, amesema kukosekana umeme katika vijiji 20, kunamkosesha usingizi na kuahidi huduma hiyo inawafikia.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Lubonde, na kuonyesha kusikitishwa kwake na ukosefu wa umeme katika vijiji hivyo kiasi cha kuonekana ni jambo la anasa ilhali ni huduma ya lazima.

"Wananchi wanahitaji umeme wa uhakika, mradi wa uzalishaji unaomilikiwa na Kampuni ya Madope Hydropower, watu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakipita wanajua sisi tayari tunao umeme, lakini bado hautoshelezi kwa sababu ni wa mgao," alisema Kamonga.

"Najua mnahitaji umeme hii ni kutengenezewa ajali ya kisiasa si ndiyo jamani? Kwa sababu wananchi watakuchukia sana kwenye vijiji vyote 20 hili jambo hata mimi linaninyima usingizi, ninahangaika usiku na mchana kushirikiana na mheshimiwa diwani wenu kuhakikisha kwamba wananchi wa kata hizi wanapata umeme wa uhakika," alisema Kamonga.

Awali, wananchi wa Kata ya Lubonde walimwomba mbunge huyo kuwaletea nishati ya umeme ya uhakika ili aweze kufanya shughuli za kimaendeleo.

"Tunakuomba mheshimwa mbunge na sisi tuletewe umeme mbona sehemu nyingine kuna umeme wa uhakika, tunashindwa kuwa na miradi ya kiuchumi kwa sababu hakuna umeme wa uhakika, huu wa Madope usiku unakuwepo mchana hakuna," alisema Philiph Kitulile.

Naye Grace Ngailo alisema changamoto ya kukosekana umeme wa uhakika ni kubwa na tatizo hilo linakwenda hadi kwenye zahanati zao.

"Sehemu kama zahanati kukosa umeme wa uhakika hii si sawa tunakua kama tupo nchi nyingine, tunamuomba mbunge wetu akaendelee kulisemea wananchi tunahitaji umeme," alisema Grace.

# ‘Tanzania inaweza kuilisha Afrika’

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya AGRA, Waziri Mkuu mstaafu wa Ethiopia, Hailemariam Dessalegn, amesema Tanzania inaweza kuilisha Afrika iwapo mapinduzi ya kilimo yatafanyika kwa umakini na kwa ukamilifu.

Akizungumza mkoani Pwani baada ya kukagua kiwanda cha kusaga mahindi kinachomilikiwa na Kampuni ya Joydons Tanzania Limited akifuatana na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, Dessalegn alieleza kuridhishwa na uwekezaji uliofanya katika kiwanda hicho na kusema:

“Nimevutiwa na uwekezaji uliofanywa katika kiwanda hiki. Tanzania inaweza kulisha nchi za Afrika endapo mapinduzi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi yatafanyika kikamilifu. Kiwanda hiki ni kielelezo cha mapinduzi hayo kwa sababu kinaongeza thamani kwenye mazao ya kilimo. Kiwanda hiki kitasaidia kuhamasisha kilimo bora katika ukanda huu,” alisema Dessalegn.

Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) na Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA) wanashirikiana katika kuimarisha kiwanda hicho ambacho kinanunua mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Pwani na Tanga na kuzalisha tani 150 za unga wa mahindi na kuusambaza mikoa mbalimbali ya Tanzania. TADB imetoa mkopo wa Sh. bilioni 1.2 kukiboresha kiwanda hicho.

Mwenyekiti wa Bodi ya TADB, Ishmael Kasekwa, alieleza ugeni huo kwamba ushirikiano kati ya TADB na AGRA umekuwa na mafanikio makubwa, na kwamba wanatumaini ushirikiano huo utaweza kuibua mageuzi yanayowaniwa katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

“Benki yetu itaendelea kutoa mikopo ili kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda inafikiwa kupitia kilimo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TADB, Derick Rugemala, alisema ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili umetokana na uhitaji mkubwa uliopo kutosheleza mahitaji ya wadau wa kilimo.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto), akionyeshwa picha ya anga ya Mji wa Tunduma inayoelezea programu ya kupanga, kupima na kumilikisha vipande ardhi na Ofisa Mipango Miji wa Mkoa wa Songwe, Joseph Towo, wakati wa uzinduzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya jana. Aliyevaa miwani ni Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Bil. 72.8/- zapeleka maji Simiyu

**Na Happy Severine,** BARIADI

MENEJA wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani Simiyu, Mariam Majala, amesema mkoa huo una miradi ya maji 178 iliyogharimu Sh. bilioni 72.8, lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo kwa wakati.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mmkoa (RCC), kilichofanyika Mjini Bariadi wakati akitoa taarifa ya hali ya huduma ya maji mkoa wa Simiyu.

Mariam alisema watu wapatao milioni 1.1 wanapata huduma ya majisafi na salama sawa na asilimia 65.8, huku jumla ya vijiji 33 kati ya 470 vikiwa havina huduma ya maji sawa na asilimia 7 ya vijiji vyote vilivyopo mkoani hapa.

Aliongeza kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, RUWASA mkoa wa Simiyu imetengewa bajeti ya Sh. bilioni 16.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kuhusu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, Mariam alisema RUWASA Mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/22 wanaendelea na maandalizi ya kujenga mradi huo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, na kwamba jumla ya vijiji 256 vitanufaika na mradi huo.

“Mradi huo utagharimu jumla ya Euro milioni 171 sawa na Sh. bilioni 444 na bomba lenye urefu wa kilomita 197 litafungwa kutoka kwenye chanzo cha maji cha Nyashimo Busega hadi Meatu, ujenzi wa mradi huo utakuwa na awamu mbili, awamu ya kwanza itapeleka maji katika miji ya Nyashimo, Bariadi na Itilima (langangabilili ) na awamu ya pili ya mradi itapeleka maji kwenye miji ya Maswa na Meatu (Mwanhuzi),” alisema.

Kwa upande wake, wananchi wa Wilaya ya Bariadi wamesema tatizo la maji bado ni kero kwa maeneo mengi, na kwamba wanaamini ujio wa mradi wa maji Ziwa Victoria utatatua tatizo hilo.

“Tunaamini mradi wa Ziwa Victoria utaokoa na kutatua tatizo la maji, kinamama wengi wanateseka sana ila kupitia mradi huo tatizo litakuwa historia,” alisema mmoja wa wananchi hao, Felister Kitama.

# Walia kwa Katambi kisa kukosa umeme

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI wa Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga, ambao wanaishi jirani na mitambo ya kupoza na kusafirisha umeme, wamelalamika kukosa huduma ya umeme kwenye makazi yao.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi.

Walisema kwenye Kata ya Ibadakuli, ndiko kuna mitambo mikubwa ya kupoza na kusafirisha umeme, lakini wakazi wa eneo hilo hawana huduma ya umeme na kuishi kwenye giza.

“Kero yetu sisi hapa mbunge ni ukosefu wa huduma ya umeme, tena cha kushangaza hapa ndiko kuna mitambo mikubwa ya kupoza na kusafirisha umeme, lakini hatuna umeme, tunaomba tupatiwe umeme,” alisema Emmanuel Martin. Naye Ofisa Uhusiano wa Huduma na Wateja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Shinyanga, Victori Senge, alisema wameshatenga Sh. milioni 61.5 kwa ajili ya kusambaza umeme mkoani humo ikiwamo Ibadakuli.

Kwa upande wake, Katambi, alilitaka shirika hilo kusambaza umeme kwa wananchi kama dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan, inavyotaka.

Alisema serikali imepunguza gharama za kuunganisha umeme majumbani kutoka Sh. 300,000, hadi Sh. 27,000.

# W’biashara wataka safari zaidi za ndege

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

BAADHI ya wafanyabiashara waliowekeza katika viwanda wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuongeza safari za ndege kwa wiki ili kuwarahisishia usafiri.

Wamesema kukosekana kwa usafiri wa uhakika kutoka Dar es Salaam hadi Kahama kunachangia kuwavunja moyo baadhi ya wafanyabiashara wanaotaka kuwekeza huko.

Wafanyabiashara hao wamesema wanalazimika kutumia muda mrefu kusafiri kwa njia ya barabara kwenda Dar es Salaam kununua vipuri mbalimbali kwa ajili ya viwanda vyao.

Akizungumzia tatizo hilo mjini Kahama, Mkurugenzi wa kiwanda cha Kahama Plastic Investment Tanzania Limited, Hamis Mhoja, alisema safari za ndege za uhakika kwa sasa haziepukiki wilayani humo.

‘’Usafiri wa ndege katika mji wa Kahama kwa sasa ni muhimu sana, kwani kuna wafanyabiashara ambao huhitaji kupata huduma mbalimbali ikiwamo kufuata vipuli vya viwandani, lakini wanashindwa kutokana na safari za ndege kuwa moja moja kwa wiki,’’ alisema.

“Tunapata wakati mgumu katika kuagiza vipuri nje kwa sisi wafanyabiashara wa viwanda kwa kuwa ndege kwa wiki inatua mara moja, hali ambayo inatulazimu kutumia usafiri wa barabara ambao unatumia siku nyingi kufika Dar es Salaam na kurudi hali ambayo inafanya kiwanda kusimama kwa muda mrefu,” alisema Mhoja.

Mhoja ambaye kiwanda chake kilifunguliwa hivi karibuni na Mwenge wa Uhuru alisema ametoa ajira 170 kwa vijana wa kitanzania na kati ya hao asilimia 40 ni wanawake na wanaume ni asilimia 60.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akiongea na Rais wa Bank of Africa, Othman Benjelloun, Rabat nchini Morocco mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kikazi nchini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walipwa mabilioni kupisha mgodi Geita

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WANANCHI 851 wa vijiji vya Mnekezi, Lubanda na Lwamgasa Mkoa wa Geita waliyokuwa wakifanya shughuli zao za kibinadamu katika eneo la mgodi wa dhahabu wa Buckreef wamethminiwa na kulipwa fidia zao zaidi ya Sh. bilioni 5.7.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, alisema TAKUKURU Mkoa wa Geita ilifuatilia miradi ya umma kwa kushiriki katika kazi mbalimbali za kijamii kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa katika shughuli hizo.

Felix alisema TAKUKURU imeshiriki katika zoezi la tathmini ya fidia kwa ajili ya upanuzi wa mgodi wa dhahabu wa Buckreef wenye ubia na serikali katika vijiji vya Mnekezi, Lubanda na Lwamgasa ambapo katika zoezi hilo jumla ya wananchi 851 waliokuwa wakifanya shughuli zao katika eneo la mgodi huo walitathminiwa na kustahili kulipwa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 5.7.

Aidha alisema pia walishiriki katika zoezi la tathmini ya nyumba zilizoathiriwa na shughuli za ulipuaji miamba katika mgodi wa dhahabu wa GGML katika mitaa inayozunguka mgodi huo uliyopo Halmashauri ya Geita Mji, ambapo jumla ya kaya 1,533 zenye jumla ya nyumba 2,800 zilitathminiwa na kustahili kulipwa zaidi ya Sh. bilioni 1.8 na zoezi la malipo linaendelea.

"Kazi zingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka 2021 ni kuendelea kupokea malalamiko kisha kufanya uchunguzi na kuendesha mashtaka ya tuhuma za rushwa mahakamani. Tumepokea taarifa za malalamiko 196 ambapo taarifa zilizohusu rushwa ni 100 na 96 hazihusiani na rushwa hivyo zilitolewa ushauri na kuelekeza walalamikaji mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao," alifafanua Felix.

Aidha, alisema sekta iliyoongoza kwa kulalamikiwa katika mkoa wa Geita ni Serikali za Mitaa malalamiko 60, sekta binafsi 37, fedha 15, madini 11, vyama vya ushirika 10, Afya 8, elimu 7, ardhi 7, maliasili 7, mifuko ya jamii 6, siasa 1, kazi 1, Polisi 5, nishati 5, biashara 4, maji 3, Mahakama 2, ujenzi 2, huduma za jamii 1, kampuni binafsi za ulinzi 1, usafirishaji 1, uvuvi 1 na dini 1.

Alisema uchunguzi wa awali wa taarifa na malalamiko yanayohusiana na rushwa umeendelea kufanyika ambapo jumla ya majalada ya uchunguzi matatu yamefunguliwa, taarifa 5 zimefungwa, taarifa 15 zimetolewa ushauri na katika kipindi hicho jumla ya majalada 7 uchunguzi wake umekamilika. Aidha, Felix alisema kesi zilizofunguliwa mahakamani ni 6 na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa mahakamani kufikia 24, ambapo kesi 6 zilitolewa maamuzi na Jamhuri kushinda kesi 5 sawa na asilimia 83 na kushindwa kesi 1.

# Mara kunufaika na mil. 68/- za NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa msaada wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 68 kwa ajili ya kusaidia sekta za elimu na afya mkoani Mara.

Msaada ambao utazinufaisha shule 11 za msingi na sekondari pamoja na Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere maarufu Kwangwa.

Msaada huo umetolewa kwa wilaya za Musoma na Rorya mkoani humu ambapo unahusisha madawati, vifaa vya kuezekea kwa sekta ya elimu pamoja na vitanda maalum kwa sekta ya afya.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kukabidhi misaada hiyo katika wilaya hizo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Juma Kimori, alisema benki yake itaendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu na afya kwa kutoa misaada ya vifaa kutokana na faida iipatayo kila mwaka.

Kimori aliongeza kuwa changamoto za sekta za elimu na afya nchini ni jambo la kipaumbele kwa benki kutokana na umuhimu wa sekta hizo katika ustawi wa jamii, na kwamba ingawa serikali imekuwa ikijitahidi kwa kiwango kikubwa kuboresha sekta hizo, lakini bado ipo haja ya jitihada hizo kuungwa mkono.

"Sisi kama wa wadau tunao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii kwani jamii hii ndio imeifanya Benki ya NMB kuwa hapa, na tutaendelea na kuunga mkono jituhada hizi ili kuhakikisha kunakuwapo na mafanikio ya hali ya juu katika sekta hizi ili ziweze kuwa mfano ndani na nje ya nchi," alisema.

Kimori alisema wameshatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.88 kuanzia Januari mwaka huu hadi sasa kuzisaidia sekta hizo, ambapo kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa, na kwamba msaada huo umezinufaisha shule na vituo vya kutolea huduma za afya 129, huku mkoa wa Mara ukiwa umepokea jumla ya madawati 587, mabati 2,580 na vitanda 8 katika kipindi hicho.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, aliishukuru kwa msaada huo huku akizitaka mamlaka husika mkoani humo kuhakikisha zinaboresha taaluma ili kuongeza ufaulu.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, Dk. Joachim Eyembe, alisema msaada huo utasaidia kuboresha huduma zitolewazo hospitalini hapo hasa ikingatiwa kuwa mwezi ujao hospitali hiyo iliyoanza kutoa huduma Novemba mwaka jana inapanua huduma zake kutoka huduma za mama na mtoto za sasa na kuongeza huduma za kibingwa.

# TFRA yashauri matumizi sahihi ya mbolea

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imesema endapo wakulima watazingatia matumizi sahihi ya mbolea watazalisha kwa wingi na kukuza vipato vyao.

Ushauri huo ilitolewa na Ofisa Udhibiti Ubora wa Mbolea kutoka mamlaka hiyo, Michael Sanga, wakatin akizungumza na Nipashe, na kusema upo umuhimu wa kuzingatia namna ya kutumia mbolea kwa ubora kwenye kilimo, na kwamba pasipo kufanya hivyo, mkulima huenda asione manufaa kupitia shughuli zake za kilimo hicho.

Alisema kabla ya mkulima kutumia mbolea anapaswa kwanza kupima afya ya udongo katika eneo analolima ili kufahamu aina na kiasi cha virutubisho vilivyomo katika udongo husika na hivyo kutumia inayoendana nao.

"Na huduma hizi zote ikiwamo za ushauri wa namna ya kutumia mbolea kwa usahihi, zinatolewa na TFRA katika Kanda zote nchini, kwa hiyo tumekuwa tukiwashauri wakulima kwamba ni vema wasipende kutumia hovyo mbolea hizi, wapende kwanza kupata ushauri na ndipo watafaidika zaidi na shughuli za kilimo," alisema Sanga.

Jambo jingine ambalo alisema wanapaswa kuzingatia ni aina ya mazao wanayopaswa kulima kulingana na aina ya udongo na kwamba kila zao huwa lina asili ya kuhitaji virutubisho vya aina yake.

"Mmea unahitaji virutuhisho 17 ambavyo ni vya msingi na upili, kwa hiyo mkulima akipanda zao bila kuzingatia haya ambayo tunasema yanahitaji ushauri kutoka kwa wataalamu anaweza asione manufaa ya shughuli zake za kilimo na atakuwa analalamika kila siku, lakini akifuata anayoelekezwa atafurahia sana kilimo," alisema Sanga.

Aliwashauri pia wakulima kuhakikisha wanakuwa makini kufuatilia na kufahamu aina ya mbolea iliyopo sokoni kwa wakati husika.

"Na wakati mwingine unatakiwa uwe makini kufahamu aina ya mbolea iliyopo sokoni kwa wakati huo, siyo unakurupuka tu eti kwa sababu unahitaji mbolea unaenda kubeba yoyote tu hapana, kwa wakulima walio makini huwa wanakuwa wanafahamu inayokuwa sokoni kwa wakati husika na ndio maana tunaendelea kusisitiza kwamba ili wakulima wapate tija kwenye shughuli zao hizo wazingatie matumizi sahihi ya mbolea na wawatumie maofisa ugani, " alisema Sanga.

Nipashe
Spotika




NYOTA 6 WANAOWANIA BALLON D'OR 2021 UK. 12-13



# NYOTA A. MASHARIKI WALIOTIKISA EURO 2020

## ISIKUPITE

KIWANGO cha fedha za mishahara ya wachezaji wa klabu ya Real Madrid kinatarajia kupungua kwa karibu pauni milioni 150 msimu huu.



**LONDON,** England

MICHUANO ya Euro 2020 imemalizika katika mjiji 11 barani Ulaya, ambapo ilishirikisha wachezaji 622 kutoka mataifa 24 barani humo.

Kizuri kati ya wachezaji hawa, wako wachezaji 55 wenye asili ya bara la Afrika ambapo wanaowakilisha mataifa ya Ulaya.

Timu ya Taifa ya Ufaransa ilikuwa na wachezaji 12 wenye asili ya Afrika akiwamo Ngolo Kante mwenye asili ya Mali, Kylian Mbappe (Cameroon) Karim Benzema (Algeria) na Paul Pogba (Guinea).

Huku Finland na Ujerumani zikiwa na wachezaji wengi pia weye asili ya Afrika. Ujerumani ilikuwa na Antonio Rudiger (Sierra Leone), Serge Gnabry (Ivory Coast), Jamal Musiala (Nigeria) na Leroy Sane, ambaye baba yake ana asili ya Senegal.

Ukiacha hao na wengine maarufu kama David Alaba nahodha wa Austria mwenye asili ya Nigeria, Bukayo Saka (Nigeria) na Memphis Depay (Ghana).

Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki nazo hazikuwa nyuma, walau na zenyewe zikiwa na wachezaji kadhaa wanaochezea mataifa ya Ulaya kwenye michuano hiyo.

Wachezaji hawa ni wale waliozaliwa Afrika wakaenda Ulaya wakiwa wadogo, ama walioasiliwa na raia wa mataifa ya Ulaya.

Waliozaliwa Ulaya kwa wazazi Waafrika kwenye makambi ya wakimbizi ama wazazi walikuwa Ulaya kutafuta maisha na wengine wamezaliwa na mzazi mmoja akiwa mwenye asili ya Afrika na mwingine ni kutoka Ulaya.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo imeomba rasmi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki inaweza kujivunia kutoa wachezaji wengi wenye asili ya nchi hiyo waliokipiga kwenye michuano ya Euro mwaka huu.

Mfano mkubwa ni wachezaji kama Steve Mandanda (Ufaransa), Michy Batshuayi na Christian Benteke (Ubelgiji) na Kelvin Mbabu (Uswisi). Ukiacha hawa wafuatao ni wachezaji wenye asili ya Afrika Mashariki wanaozibeba zaidi timu zao kwenye michuano ya Euro 2020.

**#1 Yussuf Poulsen (Tanzania & Denmark)**

Yussuf ana asili ya Tanzania, baba yake Shihe Yurary anatokea mkoa wa Tanga, alikuwa mfanyakazi katika meli za kusafirisha mizigo kati ya Tanzania na Denmark. Kwenye hizo safari akakutana na Lene Poulsen katika miaka ya 1990 na kuingia kwenye mahusiano na akazaliwa wa Yusuf mwaka 1994. Inaelezwa Shihe alifariki kwa maradhi ya saratani wakati Yussuf akiwa na umri wa miaka 6 tu.

Katika michuano ya Euro 2020, Yussuf ndiye alikuwa mchezaji mwenye asili ya Afrika kufunga bao la mapema zaidi. Alifunga dakika ya kwanza na sekunde 39 tu dhidi ya Ubelgiji.

Aliwahi kutembelea kwao Tanga kwa bibi yake mara kadhaa mwaka 1996, 2002, 2008 na 2011.

**#2 Romelu Lukaku (DR Congo & Ubelgiji)**

Lukaku ametoka kuisaidia Inter Milan kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Seria A, kwa kupachika mabao 24, na akaifungia Ubelgiji mabao manne kwenye Euro 2020.

Lukaku ni mshambuliaji wa zamani wa Manchester United ana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

**#3 Presnel Kimpembe (DR Congo & Ufarasa)**

Nyota mwingine mwenye asili ya DR Congo, aliyeiwakilisha Ufaransa. Amewahi kuichezea Timu ya Taifa ya Vijana ya DR Congo chini ya umri wa miaka 20 mchezo mmoja mwaka 2014, lakini baadaye akaamua kubeba bendera ya Ufaransa badala ya ndugu zake wa DR Congo.

Alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2018, na tangu wakati huo avae jezi za Ufaransa ameendelea kuimarika na kuwa miongoni mwa walinzi bora wa kati wanaotumika.

Amezaliwa Ufaransa baba akiwa kutoka Congo na mama kutoka Haiti na baada ya kuzaliwa akapewa jina la babu yake kama ilivyo kwa Waafrika wengi kwenye kurithi majina ya babu na bibi.

**#4 Alexander Isak (Eritrea & Sweden)**

Kijana huyu anawindwa sasa na klabu kadhaa kubwa zikiwamo Manchester United, Arsenal na Atletico Madrid. Uwezo wake unafananishwa na Zlatan Ibrahimovic, gwiji la Sweden na mshambuliaji hatari kuwahi kuchezea klabu za Inter Milan, AC Milan, Juventus, Barcelona, Ajax, Manchester United na PSG ya Ufaransa.

Isak akiwa na Sweden kwenye Euro ndiye aliyekuwa anavaa viatu vya Ibrahimovic kwenye eneo la ushambuliaji. Kinda huyu mwenye umri wa miaka 21 anayekipigia kule Real Sociedad na aliyeifungia timu hiyo mabao 33 katika misimu miwili ya ligi kuu ya Hispania (Laliga), anatoka kwa wazazi wenye asili ya Eritrea.

**5: Denis Zakaria (Uswisi & Sudan Kusini)**

Zakaria amezaliwa jijini Geneva nchini Uswisi, kwa mama kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na baba kutoka Sudan Kusini.

Anaitwa Denis Lemi Zakaria Lako Lado, kiungo mkabaji wa klabu ya Borussia Monchengladbach ya Ujerumani. Tayari ameshacheza michezo zaidi ya 30 akiwa na timu hiyo ya taifa ya Uswisi.

Lakini hakupata nafasi ya kutosha, kuonyesha cheche zake kwenye michuano ya Euro 2020.

## Extra Time

# NYOTA 6 WANAOWANIA BALLON D'OR 2021



MESSI

**LONDON, England**

TUZO ya mchezaji bora wa mwaka ya Ballon d'Or iliahirishwa mwaka jana kutokana na janga la mlipuko wa virusi vya corona, lakini inarejea tena mwaka huu, huku kukiwa na ushindani mkubwa zaidi tofauti na miaka 10 iliyopita.

Kwa kipindi cha zaidi ya muungo mmoja, ushindani ulikuwa mkubwa zaidi ukiwahusisha zaidi wachezaji wawili, Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.

Sasa baada ya kukamilika kwa mashindano mawili makubwa ya soka Dunia wiki iliyopita ya Euro 2020 na Copa America, kumetoa mwanga wa wachezaji gani wako kwenye nafasi kubwa ya kutwaa tuzo hiyo kubwa kabisa binafsi kwenye mchezo huo.

Wako wachezaji wengi waliokuwa na msimu mzuri kwenye ligi mbalimbali na kufanya vizuri pia kwenye timu zao za taifa hasa kupitia mashindano ya Copa America na Euro.

Ukiacha Ronaldo aliibuka mfungaji bora wa Euro 2020, Kevin De Bruyne aliyetwaa tuzo ya mchezaji bora England ya PFA, Gianluigi Donnarumma mchezaji bora wa mashindano ya Euro 2020 na kipa bora wa Seria A msimu huu unaoisha, wafuatao ni wachezaji 6 wanaopigiwa chapuo kushinda tuzo hiyo mwaka huu.

**#1 Lionel Messi (Barcelona & Argentina)**

Mwezi mmoja uliopita kabla ya mashindano ya Copa America usingefikiria Messi kuwa miongoni mwa wanaopewa nafasi kubwa ya kutwaa tuzo ya Ballon d'Or, lakini mashindano hayo yamempa nafasi kubwa zaidi.

Alitwaa tuzo hiyo mwaka 2019, lakini anashikilia rekodi ya kutwaa tuzo hiyo mara sita, akimpiku Ronaldo aliyetwaa tuzo hiyo mara tano.

Kinachompa nafasi zaidi Messi kwenye kutwaa Ballon d'Or ni mafanikio yake akiwa na taifa yake ya Argentina. Kwa miaka 28, Argentina ilisubiri kutwaa kombe, huku Messi akisubiri katika maisha yake kutwaa kombe la kwanza kubwa akiwa na timu yake ya taifa.

Amefanikiwa mwaka huu kwa kuipa nchi yake kombe la Copa America kama nahodha wa kweli na yeye kuibuka mfungaji bora wa mashindano, huku akitoa pasi 5 za mabao.

Katika mwaka 2021 Messi ametupia jumla ya mabao 33 na kutoa pasi za mabao 14. Amekua mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Hispania, Laliga msimu huu na mabao yake manne kwenye michuano ya Copa America yameisaidia timu yake ya Argentina kutwaa kombe hilo.

Licha ya kushindwa kuisaidia klabu yake ya Barcelona kutwaa Laliga ama Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka huu, lakini ameisaidia kutwaa Copa del Rey, hali inayomwongezea nafasi zaidi ya kutwaa tuzo hiyo mwaka huu pengine kuliko mchezaji yeyote.

**#2 Jorginho (Chelsea & Italia)**

Mara ya mwisho kutolewa tuzo hii, Jorginho alikuwa wa 15 lakini mwaka huu, kiungo huyu wa Chelsea ambaye kwa kasi yake ya kawaida anachukuliwa poa, anapigiwa chapuo la kutosha kutwaa ama kuingia tatu bora kwenye tuzo ya Ballon d'Or.

Mwaka 2021 ulipoanza hakuna hata mtu aliyefikiria kwamba angetajwa katika orodha ya wanaowania tuzo hii, lakini umekuwa mwaka wa mafanikio kwa nyota huyo wa kimataifa wa Italia akifunga mabao 7 kwenye Ligi Kuu England na kutoa pasi mbili za mabao.

Ingawa hakuwa mchezaji bora wa kuisaidia Chelsea kutwaa kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu ama Italia 'the Azzurri' kutwaa kombe la Euro mwaka huu, lakini alikuwa na mchango mkubwa unaofananishwa na Luca Modric, aliyetwaa tuzo hiyo mwaka 2018 kwa mchango wake kwa timu ya taifa ya Croatia iliyofika fainali ya kombe la dunia mwaka huo.

Tangu kutua kwa kocha Thomas Tuchel kwenye timu ya Chelsea Jorginho amekuwa akionekana kutoa mchango mkubwa katika eneo la kiungo linaoonekana kuwa imara akisaidiana na Mfaransa Ngolo Kante.

Kwa vyovyote vile taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea na la Euro 2020 akiwa na Italia yanampa nafasi zaidi kumpiku Kante ambaye alipewa nafasi zaidi kabla ya kuanza kwa mashindao ya Euro 2020 na yale ya Copa America yaliyomwongezea alama Messi.

**#3 Ng'olo Kante (Chelsea & Ufaransa)**

Ameisaidia klabu yake ya Chelsea kutwaa kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kucheza mpira wa hali ya juu hasa kuanzia robo fainali, nusu fainali na fainali alipoibuka mchezaji bora wa mechi. Mfaransa huyo alikuwa mchezaji bora kwenye mechi mbili za nusu fainali dhidi ya Real Madrid, na ile ya fainali dhidi ya Manchester City.

Mwaka 2017 na 2018 ilikuwa miaka mizuri kwa Kante, lakini 2021 umekuwa mwaka mwingine mzuri kwake unaomfanya kuwa miongoni mwa watakaoweza kuingia katika orodha ya watakowania tuzo ya Ballon d'Or.

Ingawa Mfaransa huyo mwenye miaka 30 ameshindwa kuisaidia nchi yake ya Ufaransa kufanya vyema kwenye mashindano ya Euro 2020, lakini mchango wake kwa klabu yake ya Chelsea hasa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya unamfanya kupigiwa chapuo.

**#4 Federico Chiesa (Juventus & Italia)**

Kiungo wa pembeni wa Italia, ambaye wakati huu umekuwa na mwaka mzuri katika maisha yake ya soka, licha ya kushindwa kutwaa ubingwa wa Italia mbele ya Inter Milan, lakini alisaidia Juventus kushinda Coppa Italia na Supercoppa Italia.

Licha ya kuwa Juventus imeutema ubingwa wa ligi marufu kama Scudetto baada ya miaka 9, lakini kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23, na anayeweza kucheza eneo lote la mbele kushoto kati ama kulia, amepiga soka la uhakika. Ameifungia Juventus mabao 15 katika mashindano yote na kutoa pasi za mabao 11.

Kinachomweka kwenye orodha hii ni kiwango chake kwenye Euro 2020 na kuisaidia timu yake ya taifa ya Italia kutwaa kombe hilo kwa mikwaju ya penalti dhidi ya England. Katika mashindano hayo alifunga mabao mawili dhidi ya Austria na Hispania.

Haishangazi kumuona akitajwa tajwa kuwa katika orodha ya watakaowania tuzo ya Ballon d'Or 2021, kutokana na kiwango chake kikubwa mwaka huu akiwa na Juve na timu yake ya Italia.

**#5 Harry Kane - (Tottenham & England)**

Mshambuliaji huyu wa Tottenham Hotspur, ni hatari linapofika suala la kufunga mabao. Amekuwa na msimu wa kuburudisha usio na makombe, akitwa kiatu cha dhahabu akifunga mabao 23 katika ligi kuu ya England. Kama haitoshi ametwaa tuzo ya mchezeshaji bora kwa kutoa pasi nyingi za mabao.

Kane ameiongoza pia timu yake ya England kuingia fainali ya Euro 2020 ikiwa ni kwa mara ya kwanza kabisa na fainali kubwa kwa timu hiyo kwa kipindi cha miaka 55. Alifunga mabao manne katika hatua za mtoano baada ya kuanza kwa ukame katika mechi 3 za kwanza za makundi.

Ni nahodha wa klabu na timu yake ya taifa, anachojivunia zaidi ni mafanikio binafsi ya kupachika mabao ingawa hafikiriwi kushinda, lakini anatajwa katika wale watakaoingia 10 bora.

**6# Robert Lewandowski (Bayern Munich & Poland)**

Bila shaka, huyu ni mchezaji aliye na mafanikio binafsi ya kujivunia zaidi katika ligi tano kubwa za Ulaya msimu huu. Ametwaa tuzo kiatu cha dhahabu kwa kupachika mabao mengi zaidi kwenye ligi tano bora Ulaya, kunakomfanya kumsogeza karibu katika orodha ya wanaowania tuzo ya mwaka huu ya Ballon d'Or.

Kama mwaka jana, tuzo hizi zisingeahirishwa bila shaka mshambuliaji huyu wa kimataifa wa Poland alikuwa anainyakua bila wasiwasi. Alifanikiwa kutwaa tuzo ya Mchezaji bora wa kiume wa FIFA na kua mchezaji bora wa mashindano ya mwaka huu ya klabu bingwa ya dunia. Kwa uwezo wake wa kupachika mabao kunamrejesha kweye ramani ya tuzo hiyo kwa mwaka 2021.

Amekuwa mfungaji bora wa ligi ya Ujerumani msimu uliomalizika kwa kupachika mabao 41 na kuisaidia klabu yake ya Bayern Munich kutwaa ubingwa wa ligi hiyo na michuano ya klabu bingwa ya dunia.

Kwa ujumla msimu uliomalizika, Lewandowski amepachika mabao 48 na kutoa pasi 9 za mabao. Ameifungia pia Poland mabao 3.

## Nukuu

"Hatukuwa na kikosi kibaya, ila tuliandamwa na sare nyingi mzunguko wa kwanza, hizi ndizo zimeharibu ndoto za kutwaa ubingwa msimu huu. Zilitupotezea mwelekeo, lakini ukiangalia baada ya ujio wa kocha Nabi (Nasreddine), umeibadilisha mno timu yetu na sasa imekuwa ya moto na unaona kuelekea mwishoni mwa ligi tulikuwa tukipata ushindi mfululizo." **Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela.**



"Tutafanya maboresho madogo ndani ya kikosi chetu, usajili wetu hautakuwa mkubwa sana, tunasajili wachezaji wa kimataifa wachache ili waje kusaidia kufikia malengo yetu." **Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati.**



"Ni kweli tulifanya mabadiliko, tunamtoa Francis Kahata na kumsajili Perfect Chikwende. Hajakuwa vizuri mpaka sasa kwa sababu mazingira bado yanamtatiza, kilichopo tumpe muda azoee kwa sababu ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa, atakapozoea atakuwa vizuri sana." **Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola.**





Wachezaji wa Simba wakishangilia moja ya mabao yao kwenye Ligi Kuu na kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara.

# ILIKUWA LIGI YENYE MSISIMKO, UPINZANI

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, ikimalizika jana, huku Mabingwa wa Tanzania Bara, Simba wakipewa kombe lao, baada ya kutawazwa kuwa wafalme wa soka msimu huu, lakini ikiwa ni kwa mara ya nne mfululizo.

Ilikuwa ni ligi ndefu, yenye msisimko na upinzani kwa timu zote, zilizoshiriki ligi hiyo. Pamoja na kwamba imechelewa kumalizika kuliko ligi nyingi duniani, lakini ikumbukwe kuwa Tanzania ilipatwa na msiba wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Machi 17 mwaka huu.

Hii ilisababisha michezo yote nchini, achilia mbali Ligi Kuu Tanzania Bara, kusimamishwa kwa muda wa mwezi mzima.

Pamoja na mambo mengine, kwa kiasi kikubwa, hili ndilo lililosababisha Ligi Kuu ichelewe kumalizika.

Msimu huu ligi ilionekana kugawanyika sehemu tatu. Sehemu ya tatu ndiyo iliyoonekana kuwa na ushindani mkubwa, ukiondoa timu tatu za juu, Simba, Yanga, Azam, timu zilizobaki zilionekana kufanana uwezo, kitu ambacho kilifanya ligi kuwa ngumu mno.

Kwenye makala haya, tutaziangalia timu zote zilizocheza Ligi Kuu na kushiriki wake.

**1. Simba**

Ilionekana kucheza ligi ya peke yake. Ilishinda kwa urahisi michezo yake mingi, huku ikitawala mechi. Ilikuwa kwenye kundi la peke yake.

Baada ya kufungwa mechi mbili mfululizo dhidi ya Prisons na Ruvu Shooting, Simba ilionekana kubadilika na hasa baada ya kuanza kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika. Wachezaji wake walionekana kuongezeka viwango, kiasi cha kuonekana huku nchini inacheza ligi ya peke yake, timu nyingi zikicheza kwa nia ya kusaka sare inapokutana nayo na mra nyingi hata hivyo, bado inakuwa ngumu.

**2. Yanga**

Hata Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela alinukuliwa akisema kilichowafelisha msimu huu kutwaa ubingwa na kutoa sare nyingi.

Wakati Simba ikishinda mechi nyingi mfululizo, Yanga ilikuwa ikilazimishwa sare mara kwa mara kwenye mechi ambazo ilistahili ishinde. Hata ilipojitahidi kushinda mfululizo katikati ya mzunguko wa pili, tayari ilishachelewa. Hili ni kundi la pili kwenye Ligi Kuu.

**3. Azam FC**

Ilianza kwa kushinda mechi saba mfululizo na kuongoza ligi, huku viongozi wakijinasibu kuwa msimu huu 'wana jambo lao.' Baada ya hapo timu ikaanza kusuasua. Ilianza kukaa vizuri mzunguko wa pili baada ya kuwasili kwa kocha, George Lwandamina. Azam walikuwa kwenye kundi moja na Yanga.

**4. Biashara United**

Kwa mara ya kwanza imepata tiketi ya kwenda kushiriki michuano ya kimataifa, baada ya kumaliza kwenye nafasi ya nne.

Haikuwa rahisi kwao kupata nafasi hiyo. Ilibidi itoke machozi jasho na damu.

Haikuwa na uwezo mkubwa kuliko timu zingine. Ilichozizidi ni uwezo wao wa kutumia vema uwanja wake wa nyumbani, Karume, Musoma mkoani Mara. Kuanzia hapa kwenda chini, ndipo kulikuwa na upinzani mkali kwa timu zote ambazo zilionekana kufanana uwezo, mbinu na hata viwango vya wachezaji wao. Hili ndilo kundi la tatu.

**5. Kinondoni MC**

Ilikuwa kidogo tu nayo irejee kwenye michuano ya kimataifa kama ilivyokuwa mwaka juzi.

KMC ni timu ambayo ilitoa upinzani mkali kwenye ligi, ikiwa na wachezaji wengi vijana na wenye uwezo, lakini bahati haikuwa yao.

**6. Prisons**

Timu hii inayomilikiwa na Jeshi la Magereza imekuwa moto wa kuotea mbali na msimu huu. Na hii ni baada ya kuhama Mbeya na kwenda kujichimbia, Sumbawanga mkoani Rukwa, ikicheza mechi zake za nyumbani, Uwanja wa Nelson Mandela, kiasi cha kumaliza kwenye nafasi ya sita.

**7. Dodoma Jiji**

Ni timu iliyopanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu huu. Kilichoisaidia na kuonekana ni timu ngumu na bora kama vile iko siku nyingi, ni kuwa na wachezaji wengi wazoefu ambao wamecheza Ligi Kuu kwenye klabu mbalimbali nchini.

**8. Namungo FC**

Ikumbukwe kuwa msimu huu imecheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Kinachoonekana ni kwamba kucheza michuano hiyo, huku pia ikicheza Ligi Kuu kwa wakati mmoja, huku ikiwa haina wachezaji wengi wazuri benchi ambayo wanaweza kuwasaidia wenzao, kiliwachosha na kuwa na fatiki.

9. Polisi Taanzania

Haikuwa na msimu mzuri wala mbaya sana. Pamoja na kuwa na wachezaji wenye uzoefu kama Kelvin Yondani, Marcel Kaheza na Pato Ngonyani, lakini haikutisha sana msimu huu.

**10. Ruvu Shooting**

Ruvu Shooting ni ile ile tu. Inavyoonekana ni timu ambayo lengo lake ni kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kila mwaka. Haijawahi kuonekana ikisaka walau nafasi ya kucheza kimataifa.

**11. Kagera Sugar**

Ni timu ambayo kwa misimu mitatu sasa haiko kwenye ubora wake uliozoeleka. Ikumbukwe ilishawahi kurejea Ligi Kuu kwenye 'play off' kwa kuifunga Pamba ya Mwanza msimu wa 2018/19, vinginevyo ilikuwa imeshuka.

**12. Mbeya City**

Msimu huu ilianza vibaya kwenye Ligi Kuu kiasi cha kutabiriwa kuwa ingekuwa timu ya kwanza kushuka. Mzunguko wa pili ilifanya usajili mzuri na kumleta kocha Mathias Lule ambaye angalau aliibadilisha na kuanza kupambana kubaki Ligi Kuu.

**13. Mtibwa Sugar**

Timu hii ilikuwa ikiishi kwenye Ligi Kuu kimazoea. Kwa sasa ligi imebadilika, klabu zimewekeza kwenye wachezaji bora. Hata timu ndogo nazo zinasajili wachezaji bora, tena wengine kutoka nje ya nchi. Utaratibu wa kupokea wachezaji wakongwe wanaomaliza soka lao, au kuwa na wachezaji wengi chipukizi bila ya kuwa na wenye uwezo kwa wakati huo, umeifanya timu hiyo msimu wa tatu kuwa kwenye hatihati.

**14. Coastal Union**

Inaonekana imeathirika zaidi msimu huu kwa kuondokewa na baadhi ya wachezaji wake tegemeo, Ayoub Lyanga aliyekwenda Azam FC, Ibrahim Ame aliyechukuliwa na Simba na Bakari Mwamnyeto ambaye alitua Yanga.

**15. JKT Tanzania**

Aliyeruhusu straika Adam Adam kwenda kucheza soka la kulipwa wakati bado timu hiyo inaendelea na ligi, aulizwe vizuri.

Huyu aliibeba mno timu hii. Na tangu aondoke, JKT Tanzania ilionekana ni timu ya kawaida tu. Kwa bahati mbaya nyingine ni kwamba ni timu iliyokuwa inaruhusu kufungwa mabao mengi.

**16. Ihefu FC**

Kosa lililofanywa na viongozi wa klabu hii ni kuruhusu kuendelea na wachezaji wengi wale wale waliocheza Ligi Daraja la Kwanza na kupanda Ligi Kuu.

Walikuwa wanachezaji kitoto kwenye mzunguko wa kwanza na kupoteza mechi kizembe. Mzunguko wa pili ilifanya mabadiliko na kusajili wachezaji wazoefu akiwamo Deogratius Munishi 'Dida'. Hapo ikawa afadhali.

**17. Gwambina**

Ni timu iliyoanza vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Haijulikani ni mdudu gani aliingia na kuanza kupoteza mechi nyingi kwenye mzunguko wa pili, kiasi cha kuwa hoi bin taaban.

**18. Mwadui FC**

Ndiyo timu ya kwanza kushuka daraja msimu huu. Hata hivyo ukiangalia uchezaji wao na viwango vya wachezaji hao, havitofautiani kabisa na timu zingine 14, ukiondoa Simba, Yanga na Azam, kiasi cha kujiuliza ni kwa nini ilikuwa ya kwanza kushuka, kwani nayo ilikuwa na uwezo wa kusubiri hadi mechi ya mwisho.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Erling Halaand ndio mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwa mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita, akitikisa nyavu mara 24.



# Kampuni ya upimaji ardhi yasimamishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameisimamisha kampuni ya upimaji ardhi ya Geo Plan, kuendelea na kazi kutokana na kukiuka mkataba pamoja na kuuza viwanja vya wananchi kinyume cha utararibu.

Aidha, amesema katika siku 10 za kampeni ya kusikiliza migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma, amepokea kesi 2,382 huku 500 zikitatuliwa.

Mtaka, alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata ya Mkonze, Mtaa wa Michese jijini Dodoma, kwenye mkutano wa hadhara kuhusu kero ya migogoro ya ardhi katika eneo hilo.

Kabla ya kutoa agizo hilo, Mtaka alipokea malalamiko ya wananchi ambao walilalamikia kampuni hiyo kwa madai ya kuuza viwanja vya wananchi.

Mmoja wa wakazi wa mtaa huo, John Nguvumali, alisema kuwa wamekuwa wakilalamikia kampuni hiyo kwa muda mrefu, lakini hakuna msaada walioupata kutoka kwa viongozi wao.

Alisema kampuni hiyo inatuhumiwa kudhulumu wananchi viwanja wakati wa upimaji na urasimishaji wa makazi.

"Kampuni hii inalalamikiwa sana na wananchi kutokana na kuchukua viwanja vya wananchi na kuviuza kwa watu wengine, hivyo tunakuomba mkuu wa mkoa ukiondoa hapa uondoke nayo hatuitaki," alisema.

Naye John Samweli, alisema kama kampuni hiyo itaendelea kupima viwanja katika eneo hilo itasababisha uvunjifu wa amani.

"Mkuu wa Mkoa, kampuni hii hatuitaki kwanza imefanya kazi nje ya mkataba ilitakiwa kufanya kazi hii ndani ya miezi sita, lakini hadi leo tunakwenda mwaka wa nne bado haijamaliza hii yote ni kutokana na upigaji wanaoendelea kuufanya," alisema Samuel.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu huyo akihitimisha mkutano huo, aliisimamisha kampuni hiyo kuendelea na kazi ya upimaji katika eneo hilo.

"Kuanzia leo kutokana na malalamiko haya ya wananchi, zikiwamo tuhuma za kampuni hii kujihusisha na uuzaji wa viwanja, naagiza kuacha mara moja kuendelea na zoezi la upimaji katika eneo hili," alisema Mtaka.

Aidha, alisema kazi ya upimaji kuanzi sasa itakuwa chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Jiji pamoja na Wizara ya Ardhi ili kumalizia kazi iliyobaki.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wakati ambapo Mkoa huo unapofanya jitihada za kutatua migogoro ya ardhi kuacha kujihusisha na uuzaji wa maeneo kiholela.

"Katika zoezi la kusikiliza kero ya ardhi toka julai 5, hadi leo tumepokea kesi za migogoro ya ardhi 2,382 na kesi 500 zimeamuliwa na kupatiwa majibu," alisema Mtaka.

Aliuagiza uongozi wa Jiji la Dodoma kuhakikisha kampuni ya upimaji inapolipwa fedha zake hakuna migogoro ya ardhi katika eneo linalopimwa.




Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, akizungumza kwenye uzinduzi wa ufunguaji na uchongaji wa barabara za mitaa na viongozi wa Kampuni ya Upimaji wa Ardhi Makazi Solutions (T) LTD Chilwana, Kata ya Ihumwa mkoani Dodoma, jana. Watatu kulia ni Mwenyekiti wa Bodi wa kampuni hiyo, Pazi Said. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana wapewa mbinu za kupata ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Restless Development imefanya kongamano la kuwajengea ujuzi wa kujiajiri na kuajariwa vijana wa shule za sekondari na vyuo jijini Dodoma, ili kukabiliana na tatizo la ajira. Mratibu wa Mradi wa ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa kutoka taasisi hiyo, Benetius Boniphace, akizungumza na waandishi wa habari katika kongamano hilo, alisema lengo kuu ni kuwajengea uwezo vijana kukabiliana na tatizo hilo.

"Kongamano hili leo tumewakutanisha waajiri wa sasa na wa baadaye pamoja na waajiriwa wapya ambao ni hawa vijana, ambao tumewapatia mbinu za namna ya kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwani unaweza kuta vijana walalamika hawana ajira kumbe hawana mbinu," alisema. Aidha, alisema kongamano hilo limewakutanisha vijana kutoka katika shule za sekondari na vyuo na wataalamu, wafanyabiashara, wafugaji, wajasiriamali waliofanikiwa ili kujifunza kutoka kwao. Vile vile, alisema vijana wengi wamekuwa na ndoto, hivyo wakiwapata watu waliofanikiwa katika nyanja mbalimbali watawasaidia kufikia malengo.

"Katika kongamano hilo wapo vijana wa shule ambao wanatamani kuwa madaktari, lakini wapo wanaotamani kuwa wajasiriamali wakubwa, hivyo wakikutana na watu wa namna hiyo wanaweza kuwasaidia kuwapa mbinu ambazo ziliwafikisha wao katika mafanikio na wao kutumia mbinu hizo," alisema Boniphace.

Akifungua kongamano hilo, Ofisa Maendeleo ya Jamii jijini Dodoma, Sharifa Nabalanganya, aliwataka vijana kuwa na malengo katika maisha yao iwapo wanataka kufanikiwa.

Alisema bila malengo madhubuti katika maisha yao ya shule, vyuo au katika shughuli mbalimbali hawataweza kuzifikia ndoto zao kwa wepesi.

"Malengo ni jambo la muhimu sana katika maisha ukiwa katika masomo yako, biashara au kitu chochote lazima uwe na malengo kuwa unataka kuwa nani vinginevyo huwezi kutimiza kile unacho kitaka," alisema. Pia, alisema vijana wanatakiwa kuwa waaminifu kama wataka kufanikiwa katika maisha. "Uaminifu ni kitu cha muhimu sana kwa vijana katika halmashauri zetu tunatoa mikopo ya asilimia 10, lakini kundi la vijana limekuwa ndiyo wasumbufu wakubwa katika kufanya marejesho ya mikopo yao," alisisitiza. Hata hivyo, aliwataka vijana kujituma katika shughuli zao ili kufanikiwa na kuacha kulalamika katika vijiwe. Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Geofrey Mtati, alisema amepata mbinu ambazo zitamwezesha kukabiliana na tatizo la kukosa ajira. "Awali nilikuwa sifahamu mbinu mbalimbali ambazo naweza kuzitumia kupata ajira au kujiajiri mwenyewe, hivyo kupitia kongamano hili limenufaika sana," alisema.

# TASAF yamkosha Waziri wa Zanzibar

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ( Sera, Uratibu Zanzibar), Dk. Khalid Mohamed Salum, ameeleza kufurahishwa na utekelezaji wa miradi ya mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Chamwino.

Kutokana na hali hiyo, ameahidi kuchukua ujuzi huo ili kusaidia utekelezaji wa miradi visiwani humo.

Waziri huyo alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipoongoza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kutembelea miradi inayotekelezwa na TASAF kwa walengwa wilayani Chamwino.

Alisema ujumbe wake umeenda kujifunza ili kutekeleza mpango huo kwa ufanisi kama ilivyo Tanzania Bara.

"Tumejifunza vitu vingi kwa wenzetu katika utekelezaji wa miradi ya TASAF... wanastahili pongezi kwa sababu wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa, na

sisi kwa vile ni awamu ya kwanza tumepata ujuzi wa kwenda kuboresha mpango wa utekelezaji," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamaja, alisema katika awamu ya sasa wamejipanga kujikita zaidi katika utoaji ajira za muda kwa sababu zina manufaa makubwa.

Alisema utekelezaji wa awamu ya tatu ya

mpango wamejipanga kutoa ajira za muda katika mashamba ya zabibu ambayo ni mashamba darasa.

"Hizi ajira za muda mfupi zimeleta manufaa katika awamu iliyopita kutokana na wengi wa vijana walikwenda kuanzisha mashamba yao," alisema.

Alisisitiza: "Tunafikiria katika awamu hii tujikite zaidi kufanya hivyo kwa sababu tumeona ajira za muda zinaleta matokeo chanya, walengwa wanajikwamua na kuanzisha mashamba yao binafsi."

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya TASAF wilayani Chamwino, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athuman Masasi, alisema miradi 502

imetekelezwa katika vipindi vya miaka minne kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19.

Alisema aina ya miradi iliyotekelezwa ni upanuzi, ukarabati na ujenzi wa malambo 305, vitalu vya miche ya miti ya zabibu na korosho (49), visima vifupi vya maji (17), utengenezaji wa matuta nusu duara na uvunaji wa maji ya mvua.

Miradi mingine ni udhibiti wa makongoro, uchimbaji na usafirishaji wa mitaro ya maji, mashamba darasa ya zabibu na korosho pamoja na ujenzi wa barabara.

Alisema wilaya hiyo ina jumla ya vikundi 1,077 vilivyoundwa na walengwa na kila kikundi kina walengwa kati ya 10 hadi 15 kwa ajili ya kuandaa mpango wa biashara ili waendelee kujiinua kiuchumi.







Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akikabidhi mifuko 200 kwa viongozi wa Kata za Sinde na Mwakibete jijini Mbeya mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya Shule za Sekondari Sinde na Mwakibete jijini humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC Homera aja na dawa ya utapiamlo, udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa siku 30 kwa wakuu wa wilaya zote za mkoa huo, kushirikiana na maofisa lishe wa wilaya kuandaa ratiba ya vyakula vinavyotakiwa kuliwa katika maeneo yao ili kukabiliana na udumavu na utapiamlo.

Amewataka kubandika ratiba hizo katika maeneo mbalimbali ya umma zikiwamo ofisi za kata, vijiji na kwenye taasisi za elimu ili ratiba hizo ziwafikie wazazi kupitia watoto kwa maelezo kuwa matatizo ya lishe yamekuwa yakitokana na ulaji mbovu wa vyakula.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha lishe cha Mkoa kilichofanyika jijini Mbeya na kuwashirikisha wadau wakiwamo viongozi wa serikali na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya kimataifa likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Homera alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali, hivyo ni aibu kwa kuwa na kiwango cha juu cha udumavu wa watoto ambacho ni asilimia 33.8.

"Mkishaandaa ratiba hizo, tumieni vyombo vya habari kuzitangaza na kuwaelimisha wananchi ili wawe na uelewa, tunataka ifike mahali tuachane na mijadala ya udumavu wa watoto katika mkoa wetu, ni aibu kujadili udumavu Mbeya wakati tuna kila kitu," alisema Homera.

Vilevile, aliwataka viongozi hao kufuatilia ili kujua hali ya udumavu kwenye maeneo yao ikiwamo kuzitambua familia zenye watoto wenye udumavu ili kutafuta mbinu ya kuzisaidia kukabiliana na udumavu ikiwamo kuziwezesha kiuchumi.

Alizitaka halmashauri zote za mkoa huo kuanza kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe kwa maelezo kuwa maeneo hayo ndiyo kitovu cha kukabiliana na udumavu na utapiamlo.

Awali akiwasilisha taarifa ya hali ya lishe mkoani humo, Ofisa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, alisema udumavu una madhara mbalimbali kwenye jamii, ikiwamo ukuaji duni wa kiakili na kimwili, hivyo watoto hao kuwa na maendeleo duni shuleni.

Pia alisema wanawake waliodumaa wanakuwa katika hatari ya kupata matatizo wakati wa kujifungua ikiwamo kufariki, na kwamba watoto waliodumaa wanakuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya kuambukiza.

"Lakini watoto waliodumaa wanakuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya moyo, kisukari na saratani wakiwa wakubwa, hali ambayo pia huhatarisha maisha yao," alisema Sanga.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema kiwango cha udumavu katika mkoa huo ni kikubwa kuliko kiwango cha kitaifa, hivyo viongozi wote wanatakiwa kushirikiana kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema kinachotakiwa kufanyika ni elimu kwa wananchi ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya lishe na madhara ya lishe duni ili mabadiliko yaonekane.

Alisema udumavu ni miongoni mwa vyanzo vya kukwamisha maendeleo ya taifa kwa maelezo kuwa tatizo hilo linasababisha kukosekana kwa viongozi wazuri.

Alisema mbali na tatizo la udumavu, pia mkoa huo una tatizo la watoto kuzaliwa wakiwa na uzito pungufu kutokana na mama zao kutopata lishe bora wakati wa ujauzito.

# Wasafirishaji waelekezwa tahadhari dhidi ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADEREVA na makondakta wa vyombo vya usafiri wa umma katika Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuandaa ndoo za maji tiririka na sabuni kwa ajili ya abiria wao kunawa mikono ama kuandaa vitakasa mikono.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao maalum na wadau wa usafirishaji mkoani hapa.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikitoa maelekezo kwa wananchi kujikinga na ugonjwa huo, na kwamba kila mmoja anatakiwa kujikinga na kuwakinga wengine.

Vilevile, Matei aliwataka madereva na makondakta kuepuka kujaza abiria kupita kiasi kwenye magari yao na badala yake kila gari libebe abiria kulingana na uwezo wake ili kuepuka msongamano.

"Lakini hata humo kwenye magari hakikisheni mnahamasisha abiria wenu kuvaa barakoa kwa usahihi na ikiwezekana yule ambaye hatakuwa hajavaa barakoa anatakiwa azuiliwe kuingia kwenye gari," alisema Matei.

Alisema wakati Jeshi la Polisi litakapokuwa linakagua mabasi kwenye Kituo Kikuu cha mabasi cha Mkoa huo kabla hayajaanza safari watafanya kazi pia ya kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya corona kwa abiria.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei aliwataka wadau wa usafirishaji katika Mkoa wa Mbeya kushirikiana na jeshi hilo kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu, kuharibu mali na kuwasababishia baadhi ya watu ulemavu.

Alisema jiografia ya baadhi ya maeneo ya mkoa huo ni ya miteremko na milima mikali, hivyo akawataka madereva kuchukua tahadhari wanapopita katika maeneo hayo ili kuepusha ajali.

"Lakini tutaendelea kusimamia utaratibu wa magari ya mizigo na ya abiria kutopishana kwa wakati mmoja kwenye maeneo ya milima ikiwamo pale Mbalizi, Igawilo, Mlima Nyoka na pale Mwansekwa, hii imetusaidia sana kupunguza ajali," alisema Matei. Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitangaza kuwa katika Mkoa huo wapo baadhi ya wagonjwa wa corona ambao wanaendelea kupata matibabu kwenye vituo vilivyotengwa kwa ajili ya ugonjwa huo, hivyo akawataka wananchi kuchukua tahadhari.

Moja kati ya tahadhari alizotangaza Homera ni wananchi kunawa mara kwa mara mikono kwa kutumia maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa, kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima huku akiagiza magari kuacha kujaza abiria kupita kiasi.

Aidha, aliwaagiza wakuu wa wilaya zote kushirikiana na kamati za afya za halmashauri kutoa elimu ya kujikinga na corona kwenye maeneo yao kwa kuhakikisha wanazingatia maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Afya.

# Walia kutokuwapo muuguzi wa kike zahanati ya kijiji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANAWAKE wa Kijiji cha Mulungu katika Kata ya Miombweni wilayani Mbarali, wamesema wanashindwa kwenda katika zahanati ya kijiji kupata huduma za afya ya uzazi kwa sababu zahanati hiyo haina muuguzi wa kike ambaye wanaweza kumweleza matatizo yao kwa uwazi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Anganile Luvanda, alipokuwa anasoma taarifa ya wanawake hao kwenye hafla fupi ya kukabidhiana mradi wa kisima cha maji na vyoo vya kisasa katika zahanati hiyo, uliotekelezwa na Shirika la Kimataifa la Kusaidia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wake wa SAWA.

Aliiomba serikali kukisaidia kijiji hicho kutatua tatizo hilo kwa kuajiri wauguzi wa kike ili kuwapa uhuru wanawake hao kujieleza shida zao, hastua ambayo alidai itasaidia kupunguza hata vifo vya mama na mtoto.

Alisema baadhi ya wanawake huwa wanaogopa kujieleza matatizo yao ya kiafya kwa wauguzi na wakunga wa kiume, hivyo kutopata huduma sahihi na wengine hawaendi kabisa kwenye zahanati hiyo wakiogopa kuhudumiwa na wanaume.

"Kuna baadhi ya shida za sisi wanawake huwa ni nyeti kiasi kwamba hatuwezi kuzieleza kwa uhuru tunapohudumiwa na mkunga mwanaume, hivyo tunaomba serikali itusaidie kwa kutuletea muuguzi mwenye jinsi kama sisi," alisema Anganile. Alisema ujenzi wa vyoo bora na mradi wa maji iliyotekelezwa na UNICEF, vitasaidia kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa kijiji hicho pamoja na vijiji jirani wanaohudumiwa, hivyo alilishukuru shirika hilo kwa kuwasaidia kuboresha huduma hiyo.

Akizungumzia miradi ya maji na ujenzi wa vyoo iliyotekelezwa katika zahanati hiyo, Msimamizi wa Miradi hiyo kutoka UNICEF, Mhandisi Beatus Peter, alisema katika zahanati hiyo walijenga vyoo vitatu vyenye matundu matatu kila kimoja na kwamba moja ya matundu ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Alisema baadhi ya matundu hayo yatakuwa yanatumiwa na wagongwa pamoja na ndugu wanaowauguza wagonjwa na mengine yatakuwa kwa ajili ya watumishi wa zahanati hiyo ambayo yametenganishwa kati ya wanaume na wanawake.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema tatizo la wanawake wa kijiji hicho ameichukua kwa ajili ya kuifanyia kazi.

Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutunza miundombinu iliyojengwa na serikali pamoja na wadau katika zahanati hiyo ili iwasaidie kwa muda mrefu.



# Othman ataka maslahi ya walimu kuzingatiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuzingatia maslahi na thamani ya walimu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kukuza ubora katika sekta ya elimu nchini.

Othman aliyasema hayo katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa madarasa mapya katika Shule ya Mtoni Kidatu, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema watakapowekewa walimu mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuthaminiwa katika kupata huduma za kijamii, kutawafanya kuwa na hamasa na kufanyakazi kwa bidii.

Makamu wa kwanza huyo alisema walimu wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa kazi zao, kuwajengea mazingira wezeshi ya kielimu na hata katika upatikanaji wa huduma za kijamii kutawapa uwezo wa kufanya kazi zao kwa ari.

"Hapo zamani mtu aliyekuwa na heshima kubwa katika kijiji ni mwalimu. hivyo serikali hatuna budi kuhakikisha tunamrudisha mwalimu kuwa mtu mwenye heshima na hadhi katika jamii," alisema Othman.

Aliipongeza kamati ya wazee wa shule hiyo pamoja na wadau wengine wa elimu kwa juhudi zao kubwa walizozichukua katika kuhakikisha jengo hilo linamalizika pamoja na kuwaomba kuendelea kushirikiana na serikali kuongeza nguvu na kuboresha miundombinu mbalimbali ya elimu nchini.

Aliahidi kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali katika maeneo hayo kwa lengo la kukuza maendeleo ya wananchi.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema wizara bado inaendelea kutafuta fursa mbalimbali katika kuhakikisha matatizo yanayoikumba sekta ya elimu nchini yanamalizika pamoja na kuwaomba wazee kutenga muda wa kuwashughulikia watoto wao katika masomo ili kukuza ufaulu nchini.

Akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, mjumbe wa kamati ya ujenzi, Juma Shaame Khamis, aliiomba serikali kuwasaidia kumalizia hatua iliyobaki ikiwamo utiaji wa plasta, sakafu na madirisha.

Aliiomba serikali kuwajengea jengo jingine litakalowasaidia wanafunzi wa sekondari ambao kwa sasa wanalazimika kutumia madarasa ya wanafunzi wa msingi kutokana na tatizo la uhaba wa madarasa linaloikabili shule hiyo.

Jumla ya Sh. milioni 23 zimetumika katika ujenzi wa jengo jipya la shule hiyo yenye madarasa sita na ofisi mbili za walimu.



Baadhi ya kinamama wa Shehia ya Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja wakivuna mboga walizopanda baada ya kupatiwa mafunzo kupitia mradi wa viungo uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Matatani tuhuma za kukiuka amri ya mahakama

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WATU wawili wamefikishwa Kituo cha Polisi Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa tuhuma za kukiuka amri ya Mahakama ya kuzuia ujenzi wa nyumba katika eneo la Mazizini akiwamo Mhandisi Hawa Said Natepe.

Amri ya kuzuia ujenzi wa nyumba ilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Rabia Hussen Mohamed, kufuatia kesi namba nane iliyofunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Waziri wa Ardhi Maji, Nyumba na Nishati mwaka 2020.

Watu hao walifikishwa kituo cha polisi baada ya kukamatwa wakiendelea na ujenzi wa nyumba licha ya mahakama kutoa amri ya kusitisha ujenzi mpaka kesi ya itakapomalizika na kutolewa hukumu yake.

"Tulipokea taarifa za kufanyika kwa ujenzi kutoka kwa raia mwema baada ya kupita na kuona ukifanyika na kutupigia simu na baada ya kufika tukakuta ujenzi umefika hatua kubwa na kuchukua hatua za kuripoti Polisi Mazizini," alisema Kasesa Maganga Kasesa, msemaji wa familia ya Issa Ali Issa.

Kasesa alisema kitendo cha kufanyika ujenzi licha ya Mahakama Kuu kutoa amri ya kusitisha ujenzi ni kwenda kinyume na misingi ya utawala wa sheria na kudharau amri halali ya Mahakama Kuu Zanzibar.

Alisema walilazimika kufungua kesi baada ya Januari 17, mwaka 2018 kupokea barua ya indhari ya kufutwa hatia ya matumizi ya ardhi katika kiwanja namba 475 na 476 kutoka kwa aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati, Salama Aboud Talib na kupewa mmiliki mpya Mudrik Mussa kwa mujibu wa hatimiliki namba 369 ya mwaka 2020.

Kwa upande wake Sheha wa Shehia ya Mazizini, Hassan Mohamed Mataka, alisema hakuna amri yoyote ya mahakama ya kuruhusu kuendelea kufanyika kwa ujenzi tangu kutolewa amri ya kuzuia kufanyika mpaka kesi itakapomalizika na kutolewa kwa hukumu.

"Mimi mpaka sasa sijapokea barua ya kuruhusu kuendelea kufanyika ujenzi kutoka mahakamani zaidi ya barua niliyopokea ya kuzuia kufanyika kwa ujenzi mpaka kesi itakapo malizika na kutolewa hukumu yake," alisema Sheha Mataka.

Hata hivyo, alipoulizwa Mhandisi Hawa kuhusu sakata hilo, alisema yeye sio msemaji, kampuni inayosimamia ujenzi wa nyumba hiyo na kutaka watafutwe wahusika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Awadhi Juma Haji, alisema bado hajapokea tukio hilo la kuvunjwa amri ya mahakama, lakini alisema ni kosa kwa mujibu wa sheria kuvunja amri halali ya mahakama.

Haji alisema kwa mujibu wa mihimili mitatu ya dola hakuna mamlaka yoyote yenye uwezo wa kuingilia uamuzi wa mahakama na kuwataka wananchi kujiepusha na vitendo vya uvunjaji wa sheria.

Issa Ali Issa, aliamua kufungua kesi mahakamani baada ya malalamiko yake ya kufutiwa hatimiliki na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Salama Aboud Talib, kutofanyiwa kazi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tangu kuwasilishwa Machi 6, mwaka 2018

## Tatizo mlo wenye virutubisho lapatiwa ufumbuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TATIZO la ukosefu wa mlo wenye virutubisho kwa kinamama visiwani Zanzibar limeanza kupatiwa ufumbuzi baada ya wanufaika wa mradi wa viungo kuanza kuvuna mboga na kutumia kama sehemu ya mlo wao wa kila siku jambo ambalo awali hawakuwa wakilifanya.

Hali hiyo imekuja kufuatia kuanza kwa mavuno ya mboga zenye kurutubisha lishe ambazo wanufaika wa mradi huo awali walipatiwa mafunzo ya kilimo bora na umuhimu wa kutumia mazao yao kama sehemu ya lishe.

Miongoni mwa wanufaika hao kutoka Shehia ya Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kheri Khamis Ame, alisema awali kabla ya mradi huo kuanza hawakuwa na utaratibu wa kula kile wanachokilima na waliamini wanapaswa kuuza.

Alisema licha ya kuwa mazao yao hayakua yakifanya vizuri kutokana na kukosa weledi wa njia bora za kilimo, lakini hawakuweza kutumia mboga hizo kama sehemu ya chakula chao badala yake waliuza na kupata fedha.

Alisema baada ya kupata mafunzo walifahamu umuhimu wa kula mboga na yeye kama baba wa familia hivi sasa ameanza utaratibu maalumu wa kuhakikisha kinacholimwa na kuvunwa kinakwenda nyumbani kwanza kabla ya kwenda sokoni.

"Ni mara mbili nakumbuka mke wangu alijifungua hospitali na mara zote alikuwa na upungufu wa damu baada ya kujifungua nina imani changamoto ile sasa itamalizika kwa mke wangu kwani amekua mlaji mzuri wa mboga baada ya kupatiwa mafunzo haya," alisema.

Naye Mosi Juma Ali mkazi wa Kivunge alisema kilimo cha mboga kina faida kubwa kwao na walichokikosa awali ni utaalamu na namna bora ya kuzitumia mboga hizo.

Alisema baada ya kupata mafunzo kinamama wengi wamehamasika na kilimo cha mboga ambacho kitapunguza tatizo la kinamama wengi hususani wakati wa kujifungua. Vile vile, alisema mauzo ya kilimo hicho pia yatawafanya waweze kuweka hakiba kama kikundi pia mtu mmoja mmoja na kisha kusaidia huduma za kifamilia.

Kwa upande wake ofisa lishe na uhakika wa chakula kupitia mradi wa viungo, Witness Sima William, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kila binadamu kula mboga ikiwezekana hata kila siku.

Alisema mboga ni chakula muhimu kwa binadamu na kinasaidia mfumo mzima wa urutubishaji mwilini pamoja na mmeng'enyo wa chakula jambo ambalo ni muhimu kwa maisha ya kila siku.

Mtaalamu huyo alisema kuna mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mboga kwa kuzingatia uoshaji ili virutubisho muhimu vibaki.

Mradi wa viungo unatekelezwa visiwani Zanzibar lengo ni kuwanufaisha zaidi ya watu 57,000 kutoka maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba na unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar, taasisi inayojishughulisha kusaidia maendeleo ya watu (PDF), pamoja na taasisi inayojishughulisha na utunzaji wa misitu Pemba (CFP), chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

# Hukumu mhandisi aliyeangua kilio kortini Agosti 13

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

HUKUMU dhidi ya Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji, Mhandisi Rahel Buliba (38), anayedaiwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 75 iliyoshindikana kutolewa kutokana na mtuhumiwa kuangua kilio mahakamani sasa itatolewa Agosti 13, mwaka huu, katika Mahakama ya Wilaya ya Geita.

Baliba alikuwa akifanyakazi katika Halmashauri ya Geita na kesi yake ilishindwa kuendelea kwa upande wa Jamuhuri kumuhoji, kutokana na kuangua kilio alipoulizwa kuhusu mzazi mwenzake ambaye inadaiwa akaunti yake ilitumika kupitisha fedha hizo.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda, ililetwa mahakamani kwa ajili ya upande wa Jamhuri kuendelea kumuuliza maswali mshtakiwa huyo.

Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba na upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri na Wakili wa Serikali, Daniel Masambu.

Mahojiano ya wakili Masambu na mshtakiwa yalikuwa kama ifuatavyo;

**Wakili:** Mara ya kwanza ulikuwa umeshtakiwa na wenzako wawili?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Wote kwa pamoja na wenzako wawili mlishtakiwa kwa makosa ya rushwa?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Wenzako wawili walikiri makosa ya rushwa?

**Shahidi:** Mimi sifahamu kama walikiri makosa.

**Wakili:** Nitakuwa sawa sawa kwamba washtakiwa wenzako wawili walikiri makosa yao?

**Shahidi:** Utakuwa sawa sawa.

Mahojiano kati ya Wakili Mashimba na mshtakiwa yalikuwa kama ifuatavyo;

**Wakili:** Barua ya kuongeza mradi wa kusambaza mabomba ya maji aliandika nani?

**Shahidi:** Mkurugenzi.

Wakili: Barua ukishaandika huwa unaipeleka wapi?

**Shahidi:** Kwa Mkurugenzi anaipitia kisha anaisaini.

**Wakili:** Fedha za rushwa zilingizwa lini benki?

**Shahidi:** Ni tarehe 13/3/2014.

**Wakili:** Mawasiliano ya mume wako Edes na watu wengine yako vipi?

**Shahidi:** Mimi sifahamu.

Mshtakiwa huyo na wengine wawili wanakabiliwa na makosa tisa ya uhujumu uchumi na rushwa ya Sh. milioni 75 za mradi wa maji wa vijiji viwili ambavyo ni Chikobe na Nyamtukuza.

Washtakiwa Edes Joseph na Frasinci Nyenge walikiri makosa yao yote na kuhukumiwa kwenda jela miaka 4 au kulipa faini ya Sh. milioni 75 na washtakiwa hao kwa pamoja walilipa faini na kuachiwa huru.

Awali, hati ya mashtaka iliyowasilishwa mahakamani humo ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo na wenzake walitenda makosa hayo Machi na Oktoba mwaka 2014 kwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 75 kupitia kwenye akaunti ya mzazi mwenzake, Edes Joseph kutoka kwa mkandarasi, Francis Nyenge ili apate kuongezewa muda wa mkataba wa kusambaza mabomba ya maji katika mradi huo.



Watoto wakifurahia kwa kutembea ufukweni mwa Bahari ya Hindi wakiwa kwenye farasi juzi, kwenye ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# EWURA yapewa jukumu bomba la mafuta

**Na Restuta Damian, MISSENYI**

WAZIRI wa Nishati, Medard Kalemani, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kusambaza ofisi kwenye maeneo ambayo miradi ya serikali inatekelezwa ili kusaidia kampuni za ndani kupata usajili wenye kuzitambua na kupewa nafasi za ushiriki wa kazi zinazotolewa.

Kauli hiyo ilitolewa jana katika kikao na wadau wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kilichofanyika wilayani Misseny mkoani Kagera, ambayo ni wilaya itakayopitiwa na bomba hilo likitokea Hoima nchini Uganda hadi Tanga kupita mikoa nane nchini.

Kalemani alisema, shughuli za mradi wa bomba la mafuta zinatarajia kuanza baada ya kukamilisha zoezi la fidia kwa wananchi walioguswa kwenye maeneo yao na ushiriki wa kampuni za ndani za kitanzania kupatiwa fursa zaidi.

"Hapa tu nisisitize EWURA toeni usajili wa kampuni za ndani tena za kitanzania zitambuliwe na zipewe nafasi na ushiriki wa kazi zitakazokuwa zikifanyika wakati wa utekelezaji wa mradi wa mafuta ghafi, kwani ukiangalia ndani ya mikoa minane bomba linapita," alisema Kalemani.

Aidha, alisema ajira mbalimbali zitatolewa na Watanzania zaidi ya10,000 watapata fursa ya ushiriki, na kwamba kampuni zaidi ya 300 zimepatiwa usajiri wa EWURA ili kupatiwa kazi.

Alisema, katika makubaliano ya mkataba wa manufaa ya mradi huo bkati ya Tanzania na Uganda, zilipeana asilimia 15 kwa kila nchi na serikali kutoa mchango wa Sh. bilioni 259.96 ambayo ni sehemu ya ushiriki wa ujenzi wa mradi huo.

Alisema ujenzi utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu baada ya ulipaji wa fidia, hivyo kazi kuukamilika mwaka2024.

Mkurungenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Dk. James Matarajio, alisema hadi Juni mwaka huu, fidia kwa wananchi ilianza kutolewa kwenye mikoa inayopitiwa na bomba hilo.

Alisema mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga hadi kufikia mwishoni wa mwezi Julai mwaka huu, zoezi la ulipaji fidia utakuwa umekamilika.

Mwakilishi wa EWURA, Kenneth Kaganga, alisema katika kusajili kampuni kuna vigezo vya sifa ya mzawa ambavyo vitaangaliwa na Mamlaka kupitia Kampuni ya Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA).

Aliongeza sajili za kampuni za umeme, ujenzi, huduma za logistic na usafirishaji, vyakula, maradhi, fedha na bima umeshafanyika na kuongeza fursa za upataji nafasi za kazi kupitia udhibiti wa mamlaka za serikali.

## DC apigia debe kilimo cha pamba

**Happy Severine, BUSEGA**

MKUU wa Wilaya ya Busega, Gabriel Zakaria, amewataka viongozi wa vijiji, watendaji, viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) na maofisa ugani kuhamasisha wakulima wa zao la pamba walime kilimo chenye tija ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Zakaria alisema hayo jana alipokuwa akipokea majumuisho ya uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya uongezaji tija zao la pamba katika uzinduzi uliofanyika katika Wilaya ya Busega.

Vijiji 23 vinatarajiwa kufikiwa na wahamasishaji kutoka Bodi ya Pamba.

Awali akitoa majumuisho ya kampeni hiyo katika Wilaya ya Busega, balozi wa zao la pamba kitaifa, Aggrey Mwanri, alisema walikutana na kero kwa baadhi ya vijiji kukosa watendaji na kusababisha kushindwa kusomewa taarifa za mapato.

Mwanri alisema ili kufikia lengo la uzalishaji wenye tija, ni vyema wakulima wakazingatia elimu kwa kutumia kipimo cha CM 60 kwa CM 30, matumizi ya samadi na namna bora ya upuliziaji wa dawa katika mashamba yao.

Naye Ofisa Kilimo Mkoa wa Simiyu, Kija Kayenze, alisema kampeni hii ya uhamasishaji na uongezaji tija katika zao la pamba mkoani humo.

Aidha, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Rukungu Kata ya Lamadi, Regina Kamongo, aliahidi kuwa kijiji chake kinafikia lengo la kuzalisha tani 200 kwa kutumia kipimo cha CM 60 kwa CM 30.

Akifunga semina hiyo mkuu huyo wa wilaya alisema ni jukumu la kila ofisa kilimo kufika kwa wakulima, na kwamba vijiji vitano vitakavyoongoza kwa uzalishaji wa zao hilo vitapatiwa tuzo katika msimu ujao.

**Awali akitoa majumuisho ya kampeni hiyo katika Wilaya ya Busega, balozi wa zao la pamba kitaifa, Aggrey Mwanri, alisema walikutana na kero kwa baadhi ya vijiji kukosa watendaji na kusababisha kushindwa kusomewa taarifa za mapato.**

HABARI KIMATAIFA

# 7 wauawa Uganda mpakani mwa DRC

**Kampala, UGANDA**

WIZARA ya Ulinzi Uganda, imesema mwanajeshi mmoja ni miongoni mwa watu saba waliouawa baada ya kutokea kwa mapigano kati ya wanajeshi na watu wenye silaha, mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Msemaji wa Jeshi la Uganda, Brigedia Flavia Byekwaso, ameliambia Shirika la Habari la Ufaransa AFP kwamba, watu wenye silaha wapatao 20, waliojifanya wafanyakazi wa misitu, waliwashambulia wanajeshi wa Uganda katika msitu wa Zeu, katika mpaka wa nchi hizo mbili.

Ilibainika, miongoni mwa watu hao wenye silaha, sita walikuwa kutoka kabila la Lendu na wengine wanne wamekamatwa.

Jeshi la Uganda lilisema mbali na kumpoteza ofisa wake mmoja, katika mapambano hayo ya siku ya Ijumaa wiki iliyopita, maofisa wake watatu, walijeruhiwa na kukimbizwa jijini Kampala kupata matibabu.

Machi, mwaka huu, watu wenye silaha kutoka DRC waliwateka wavuvi 16 kutoka Uganda katika Ziwa Albert.

Mwezi Aprili mwaka jana, wanajeshi wa Uganda, waliwaua wanajeshi watatu wa DRC waliodaiwa kuvuka mpaka na kuingia Uganda na kuanza kuwashambulia wakazi wanaoishi karibu na Ziwa Albert, ambalo lina hifadhi ya mafuta.

RFI



Daraja lililoharibiwa eneo la Ahrweiler, Magharibi mwa Ujerumani kutokana na mvua kubwa zilizosababisha mafuriko nchini humo na eneo la Ulaya. Hadi jana vifo takribani 180 viliripotiwa nchi kadhaa za Ulaya. **PICHA: AP**

# Mafuriko Ujerumani yaongeza idadi ya vifo

**North Rhine-Westphalia, UJERUMANI**

VIFO vinazidi kuongezeka wakati Ujerumani ikitafakari uharibifu uliosababishwa na mafuriko.

Rais wa Ujerumani Frank-Walter Steinmeier, aliwatembelea waathiriwa wa mafuriko hayo.

Rais Frank-Walter Steinmeier, ametembelea Jimbo la North Rhine-Westphalia ambalo limeathirika zaidi na mafuriko.

Alisema baada ya mkutano na waokoaji katika mji wa Erftstadt watu wengi wamepoteza kila kitu walichokuwa nacho kwenye maisha yao, ikiwamo nyumba na vitu vingine.

Zaidi ya watu 140 wamekufa katika eneo la Magharibi mwa Ujerumani, huku vifo zaidi vikiripotiwa barani Ulaya kote.

Watu wengine 670 wamejeruhiwa katika mafuriko hayo, taarifa ya polisi ilisema watu wengi bado hawajulikani walipo.

Serikali ya Ujerumani, iliwapeleka wanajeshi 850 kusaidia katika maafa hayo yaliyotokea.

Kansela Angela Merkel, atatembelea maeneo yaliyokumbwa na mafuriko ili kujionea uharibifu na kukutana na waathiriwa, baada ya siku kadhaa za mvua kubwa zilizonyesha katika maeneo ya Ulaya Magharibi. Merkel alikwenda katika kijiji cha Schuld katika Jimbo la Rhineland-Palatinate, mojawapo ya maeneo mawili yaliyoathirika zaidi Magharibi mwa Ujerumani.

Mkoa wa Upper Bavaria, ambao uko katika Jimbo la Kusini mwa Ujerumani, pia unashuhudia hali za dharura.

Wazimamoto wamepelekwa katika eneo hilo kukabiliana na barabara zilizojaa maji na maporomoko ya ardhi katika mkoa huo.

Wakati maji ya mafuriko yanaendelea kupungua sehemu nyingi zilizoathiriwa zimeweza kufikiwa na hivyo kujionea kiwango cha uharibifu kilichotokea.

Waziri wa Fedha wa Ujerumani, Olaf Scholz, pamoja na Waziri wa Uchumi Peter Altmaier, wameahidi msaada kwa waathirika wa mafuriko hayo.

*DW*

# Tangi la mafuta lalipuka, laua 13

**Kisumu, KENYA**

WATU 13 wamefariki dunia baada ya tangi la mafuta ya petroli kulipuka, Magharibi mwa Kenya, usiku wa kuamkia jana.

Ajali hiyo imeripotiwa kutokea wakati dereva alipojaribu kupishana na lori lingine katika barabara ya Kisumu na Busia.

Watu hao walikimbilia eneo la tukio wakiwa na madumu ya kujimiminia mafuta wakati lori hilo lilipopinduka, ghafla likawaka moto.

Watu wapatao 11 wakiwamo watoto, wapo hospitalini wakiwa na hali mbaya baada ya kuungua.

Iliwachukua saa mbili kwa kikosi cha zimamoto kufika katika eneo la tukio karibu na mji wa Malanga katika kaunti ya Siaya, kilomita 315 Kaskazini-Magharibi mwa mji mkuu wa Nairobi.

"Hatukuweza kupata kituo za kuzima moto kaunti ya Siaya kwa kuwa ni Nairobi," ofisa polisi Moreso Chacha alisema.

"Vikosi wa kuzima moto vilitokea katika kaunti za jirani."

Lori lilikuwa limebeba maziwa kutoka Busia, karibu na mpaka wa Uganda kuelekea Kisumu, wakati lilipogongana na lori la mafuta lililokuwa linaelekea eneo tofauti, kamanda wa polisi alisema.

Ajali za barabarani si jambo geni katika mataifa ya Afrika Mashariki, ambapo malori na magari mengine yanapogongana kutokana sababu mbalimbali ikiwamo ya mwendokasi.

Watu wapatao 3,000 hufariki kutokana na ajali za barabarani, kila mwaka, Kenya.

*BBC*

# Papa Francis asalimia waumini wake baada ya siku 14 upasuaji

**Vatican City, ITALIA**

WIKI mbili baada ya Papa Francis kufanyiwa upasuaji wa utumbo mkubwa, amerejea katika shughuli zake na kuonekana hadharani kuwasalimu waumini wake.

Waamini wake walimpungia mkono na kuinua bendera za taifa baada ya kumwona Papa Francis jana.

"Ndugu zangu, dada na kaka, ni siku njema," Papa Francis alisema huku akitabasamu kwenye eneo lililojaa umati la St. Peter.

Papa Francis alilazwa kwenye Hospitali ya Kikatoliki iliyopo mjini Roma, Vatican City katika Hospitali ya Gemelli, Roma kwa upasuaji wiki chache zilizopita, uliopangwa awali akiwa na dalili ya ugonjwa wa 'colon diverticulum stenosis'.

Kiongozi huyo wa kiroho mwenye umri wa miaka 84 kufanyiwa upasuaji huo ni mara ya kwanza tangu achaguliwe kuwa Papa mwaka 2013.

**AP**

# Mjane wa Rais Haiti arudi nyumbani

**Port-au-Prince, HAITI**

MJANE wa Rais aliyeuawa Haiti Jovenel Moise, Martine amerudi nyumbani baada ya kutibiwa majeraha aliyoyapata katika shambulio.

Waziri wa Mawasiliano wa Serikali Frantz Exantus, kupitia mtandao wa twitter aliandika kwamba Martine Moise, alipokelewa katika uwanja wa ndege wa Port-au-Prince na Waziri Mkuu wa mpito Claude Joseph.

Martine alilazwa katika Hospitali ya Miami, Florida, Marekani kwa siku 10 baada ya kushambuliwa pamoja na mumewe nyumbani kwao, Rais aliuawa kwa kupigwa risasi, Julai 7, mwaka huu.

Mazishi ya kiongozi huyo yanatarajiwa kufanyika Julai 23, mwaka huu, Cap-Haitien, jiji la kihistoria, Kaskazini mwa Haiti, ambalo limeathirika vibaya na machafuko tangu kuuawa kwa Moise.

**DW**

# CANNAVARO:
## Donnarumma atakuwa bora miaka 15

**ROME, Italia**

GIANLUIGI Donnarumma ni mshindi wa Euro 2020 na Italia na atakuwa golikipa bora duniani kwa miaka 10 hadi 15 ijayo, kwa mujibu wa Fabio Cannavaro.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 alitajwa kuwa mchezaji bora wa mashindano ya Euro 2020 baada ya kuibuka shujaa kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti dhidi ya England kwenye fainali pale katika dimba la Wembley.

Donnarumma aliokoa penalti za Jadon Sancho na Bukayo Saka, baada ya Marcus Rashford kugonga mwamba, wakati Italia ikimaliza ukame wa miaka 53 ya kusubiri kulitwaa taji la Ulaya kwa mara ya pili.

Gwiji wa Italia, Cannavaro anaamini Donnarumma amejipambanua mwenyewe kwa kiwango alichokionyesha kwenye mashindano ya Euro 2020 na anatarajia kwamba atang'ara zaidi kwa kipindi cha muongo mmoja ujao.

"Donnarumma ni bingwa halisi kwa kikosi hiki cha Azzurri," alisema Cannavaro akiiambia Tuttosport. "Sishangazwi na hilo, kabla ya Euro, watu walidhani ni golikipa wa kawaida.

"Ameonyesha kiwango cha hali ya juu na sina wasiwasi na Gigio. Kwa umri wake wa miaka 22 atakuwa golikipa bora kwa miaka 10 hadi 15 ijayo."

Donnarumma alicheza dakika nyingi zaidi kwenye Euro 2020 kuliko mchezaji yoyote (719), akikosa mchezo wa makundi wakati Italia ikishinda dhidi ya Wales.

Baada ya kung'ara na kikosi hicho, kipa huyo kijana alikamilisha usajili wa kujiunga na Paris Saint-Germain akitokea AC Milan, ambako atashindana na Keylor Navas.

"Angalau tutamshuhudia kwa muda mrefu zaidi kwenye timu yetu ya taifa," aliongeza kusema Cannavaro.




# ARTETA ASEMA SURA MPYA ZINATUA ARSENAL

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amethibitisha kwamba, Arsenal wapo kwenye nafasi ya kusajili sura mpya baada ya timu yake kutoka sare ya 2-2 na Rangers kwenye mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya.

Nuno Tavares, ambaye alisajiliwa kutoka Benfica, alifunga bao lake la kwanza akiichezea kwa mara ya kwanza Arsenal, na straika Eddie Nketiah pia alifunga.

Arsenal wanatajwa kukaribia kumsajili mlinzi wa kati, Ben White kutoka Brighton and Hove Albion kwa ada ya pauni milioni 50, wakati Arteta akiangalia uwezekano wa kuimarisha safu yake ya ulinzi.



Tangazo la usaili huo lilitolewa wakati Arsenal ikiwa inajiandaa kwenda nchini Marekani kuweka kambi pale Florida, ingawa imeripotiwa kwamba, White kwa sasa yupo likizo.

"Tutakuwa na sura mpya zitakazokuja hivi karibuni, kila kitu kinakwenda sawa," alisema Arteta baada ya timu yake kupata sare hiyo kule Glasgow.

"Timu itakuwa na sura nyingi na pengine zingine zenye majina makubwa, hivyo tunaamini timu itakuwa katika kiwango cha kuvutia kabisa."

Aidha Arteta alionyesha kuridhishwa na kiwango cha Arsenal kwenye mchezo huo wa Jumamosi, lakini alidokeza kutofurahishwa na namna walivyoruhusu mabao ya Rangers.

# Al Ahly yabeba taji la 10 Afrika

**CASABLANCA, Morocco**

AL Ahly imeweka historia ya kuwa klabu ya kwanza barani Afrika kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Afrika mara 10.

Hiyo ni baada ya ushindi wa mabao 3-0 walioupata Al Ahly juzi usiku dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Dimba la Mohammed V nchini Morocco.

Ahly na Kaizer ziliingia hatua ya fainali baada ya kuzitoa Esperance ya Tunisia na Wydad Casablanca ya Morroco.

Katika mchezo wa juzi, dakika 45 za kipindi cha kwanza zilikuwa bora zaidi kwa timu zote mbili kucheza kwa nidhamu kubwa ya kujilinda.

Lakini Kaizer walipata pigo baada ya mchezaji wake, Happy Mashiane kupata kadi nyekundu kwa kucheza faulo kabla ya timu hizo kwenda mapumziko.

Kipindi cha pili kilirejea kwa Ahly kutumia vyema fursa ya Kaizer kuwa pungufu uwanjani na kufanikiwa kufunga mabao matatu yaliyowapa taji la 10 katika fainali 14 walizocheza.

Mabao hayo ya Ahly yalipatikana kupitia kwa Mohamed Sherif aliyefunga dakika ya 53, Mohamed Afsha dakika ya 64 na Amr El Solia aliyegongelea msumari wa mwisho dakika ya 74.



## HABARI MICHEZO

# Jimenez arudi rasmi dimbani

**LONDON, England**

RAUL Jimenez amerudi kuichezea Wolves baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu wakati fowadi huyo wa Mexico alipoanza katika mchezo wa Jumamosi wa kirafiki dhidi ya Crewe Alexandra.

Jimenez amekuwa nje ya dimba tangu alipoumia kichwa alipogongana na mlinzi wa Arsenal, David Luiz, Novemba mwaka jana.

Mchezaji huyo wa zamani wa Benfica mwenye umri wa miaka 30 alirudi kuanza mazoezi Mei mwaka huu, miezi sita baada ya kufanyiwa upasuaji wa kichwa.

Alibainishwa kwamba yupo tayati kurudi uwanjani dhidi ya Crewe, akianza kwenye kikosi cha kwanza cha Wolves ukiwa ni mchezo wa kwanza chini ya kocha mpya, Bruno Lage.

Jimenez amekuwa na kiwango cha kuvutia sana kwa Wolves tangu walipopanda daraja kuja kwenye Ligi Kuu ya England, akifunga mabao 30 katika mashindano yote katika misimu yake miwili ya kwanza na klabu hiyo.

Alifunga mabao manne katika msimu wa 2020-21 kabla ya kuumia pale kwenye dimba la Emirates.




# ARTHUR

## afanyiwa operesheni ya goti

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imethibitisha kiungo wake, Arthur atakosa mwanzo wa msimu wa Serie A baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa wiki chache za mwanzo wakati Juve wakianza kampeni ya kurudisha taji la Scudetto lililotwaliwa na Inter Milan msimu uliopita.

Juventus wataanza msimu mpya ugenini dhidi ya Udinese, Agosti 22.

Nyota huyo alitua Juve akitokea Barcelona Juni 2020 - dili ambalo lilimhusisha Miralem Pjanic kwenda upande mwingine na Arthur amecheza mechi 32 kwenye mashindano yote katika msimu wake wa kwanza na Bianconeri hao.

Kiungo huyo wa kati alifunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo wakati wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Bologna, Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 aliumia goti wakati kikosi chake kikicheza na Atalanta, lakini aliamua kusubiri kufanyiwa operesheni hadi msimu umalizike.

Na sasa klabu hiyo imethibitisha kupitia kwenye tovuti yao rasmi kuwa operesheni hiyo imefanikiwa na anaweza kukaa nje kwa miezi mitatu.

Juventus msimu unaokuja watakuwa chini ya kocha, Massimiliano Allegri, ambaye amerudi baada ya kuiongoza timu hiyo kwenye ushindi wa Scudettos mara tano mfululizo na fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya, mwaka 2014 na 2019.




# Varane, Man United wakubaliana

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imefikia makubaliano ya maslahi binafsi na wawakilishi wa mlinzi wa Real Madrid, Raphael Varane.

Mara makubaliano ya mwisho yatakapofikiwa, itawawezesha United kukamilisha kwa haraka makubaliano ya ada na Real Madrid kwa ajili ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwenye kikosi chao.

Man United wanapambana kuhakikisha wanakamilisha usajili wa mchezaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Varane mwenye umri wa miaka 28 ameonyesha nia ya kutaka kuondoka pale Real Madrid ambako mkataba wake wa sasa unafikia tamati msimu ujao wa kipindi cha majira ya joto.

Varane amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora zaidi tangu alipojiunga na Real Madrid akitokea klabu ya Lens ya nchini Ufaransa kipindi cha majira ya joto mwaka 2011.

Ameichezea klabu hiyo jumla ya mechi 350 kwenye mashindano yote na pia akicheza mara 79 kwa Timu ya Taifa ya Ufaransa akiisaidia kubeba taji la Dunia mwaka 2018 na alianza katika mechi zote nne kwenye mashindano ya Euro 2020 kabla ya kutupwa nje na Uswisi.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti ya Daily Mail, Varane ameshakubaliana na mashetani wekundu hao ambao sasa wakati wowote wanaweza kutuma ofa ya kumsajili ili akakipige pale katika dimba la Old Trafford.



HABARI MICHEZO

## KWA UFUPI

### CHELSEA YAMTAKA LEWANDOWSKI

CHELSEA itaangalia uwezekano wa kumsajili straika wa Poland, Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich kwa kiasi cha pauni milioni 50 - ingawa mabingwa hao wa Ujerumani wanataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kuongeza mkataba wake, ambapo wa sasa unamalizika mwaka 2023. ***(Sun)***

### ALISSON KUONGEZA MKATABA

GOLIKIPA wa Liverpool, Alisson raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 28, anakaribia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu. (Mirror)

### ARSENAL WAMTAKA LOKONGA

ARSENAL inamatumaini ya kukamilisha usajili wa pauni milioni 18 kumchukua kiungo wa Anderlecht, Albert Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail)***

### GALLAGHER KUONDOKA

KIUNGO wa Chelsea, Conor Gallagher ataruhusiwa kuondoka kwa mkopo msimu huu, huku Crystal Palace na Newcastle United zote zikiwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Sun)***

### MAN RASMI KWA VARANE

MANCHESTER United wanatarajia kutoa ofa rasmi kwa Real Madrid ili kumsajili mlinzi, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28 wiki hii. ***(Daily Mail)***

### VARANE AGOMBEWA

MLINZI wa pembeni wa Ufaransa na Real Madrid, Raphael Varane anayewindwa na Manchester United pia anawaniwa na Chelsea na Paris St-Germain. ***(Marca)***

### KANE KUTOHUDHURIA MAZOEZI

WACHEZAJI wenzake na Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, wanaamini nahodha huyo wa England hatakuwapo kwenye mazoezi ya kikosi hicho ya kujiandaa na msimu mpya, kwani analazimisha kuondoka na kujiunga na Manchester City kipindi hiki cha majira ya joto. ***(The Telegraph)***

### SPURS NA PELLEGRINI

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili nyota wa AS Roma, Lorenzo Pellegrini mwenye umri wa miaka 25, ingawa hawana uhakika kama kiungo huyo wa Italia atakuwa tayari kuhamia England. ***(Gazzetta dello Sport via Sport Witness)***

### YARMOLENKO AWANIWA

FENERBAHCE wapo kwenye mazungumzo na West Ham United juu ya dili la pauni milioni mbili ili kumsajili winga wa Ukraine, Andriy Yarmolenko mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***

### HENDERSON NA MKATABA

KIUNGO wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 31, anatarajia kusaini mkataba mpya na Liverpool. Mkataba wa sasa wa nahodha huyo wa wekundu hao hapo Anfield unamalizika mwaka 2023. ***(Mirror)***

### TELLES HAONDOKI MAN

MLINZI wa kushoto wa Brazil, Alex Telles, amekanusha taarifa kwamba anaweza kuondoka Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto akisema kwamba, "nia yake" ni kuendelea kucheza hapo Old Trafford. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye alijiunga na United akitokea Porto mwaka jana, amekuwa akihusishwa na Roma na Inter Milan. ***(Goal)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GIROUD: NATAKA MATAJI NA MILAN

...Aitaja kuwa ndio timu iliyoibua ndoto yake akishabikia tangu akiwa mtoto...

**MILAN, Italia**

OLIVIER Giroud amesema kwamba, anataka kushinda mataji akiwa na timu yake mpya ya AC Milan, baada ya kusajiliwa rasmi, juzi.

Raia huyo wa Ufaransa alikamilisha usajili huo akitokea Chelsea na amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuwachezea miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Na sasa nyota huyo amebainisha kwamba, kiu yake ni kushinda mataji akiwa na timu yake hiyo mpya.

"Najihisi kama mtoto mdogo, miaka 35 au zaidi ya 35 sio tatizo," alisema Giroud akiiambia Milan TV.

"Wakati nilipokuwa kijana mdogo, nilikuwa napenda kuwaangalia Jean-Pierre Papin, Andriy Shevchenko na pia Paolo (Maldini).

"Timu hii ndio iliyotengeneza ndoto yangu. Pia nilikuwa shabiki mkubwa wa Marco van Basten. Hivyo wachezaji wakubwa wengi wamecheza hapa katika klabu yenye historia kubwa barani Ulaya.

"Milan wana historia ya kuvutia Ulaya na ndio maana nilitaka kujiunga na klabu hii ambayo nina mapenzi nayo kwa muda mrefu.

"Pia kucheza kwenye mashindano makubwa Ulaya, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na nina matumaini tunaweza kufanikisha mambo mengi na timu hii."

Milan itarudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2013-14.

Ni Real Madrid pekee imeshinda mara nyingi (13) taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikifuatiwa na Milan ambayo imeshinda taji hilo mara saba, lakini Rossoneri hao hawajatwaa tangu mwaka 2007.

Baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa akiwa na Chelsea, Giroud sasa anataka kufanya hivyo pia akiwa na Milan.

"Kama nimebarikiwa nafasi ya kushinda mataji, nikichezea klabu kubwa, basi nitafanya hivyo," aliongeza Giroud.

"Nafikiri Milan ni klabu ambayo inastahili kucheza kwenye daraja la juu kabisa."

Giroud anatarajiwa kucheza pamoja na straika mkongwe, Zlatan Ibrahimovic katika klabu hiyo.

# SIMBA QUEENS WAHITAJI MECHI TATU KUJIFUA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema anahitaji mechi tatu za kirafiki za kimataifa kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ya Wanawake kanda ya Baraza la vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Michuano hiyo iliyotarajiwa kufanyika Jumamosi, lakini iliahirishwa na sasa imepanga kufanyika Agosti Mosi, 2021, nchini Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mgosi alisema baada ya mapumziko ya siku tatu leo timu inaingia kambini na kufanya mazoezi mara mbili kwa siku kwa ajili ya maandalizi ya michuano hiyo.

Alisema watatumia wiki ya kwanza kwa ajili ya mazoezi na baadae watakuwa na mechi za kirafiki za kimataifa huku wakipambana kupata timu kutoka nchini Burundi, Kenya au Uganda.

"Kesho (leo) tunaingia kambini, nahitaji mechi za kirafiki za kimatafa zisizopungua tatu, kwa sasa tunapambana kutafuta timu katika mataifa matatu, nina imani tukikosa basi hata moja ili tupate maandalizi mazuri," alisema Mgosi.

"Tunaendelea kubakia hapa Dar es Salaam kwa ajili ya kambi na maandalizi ya michuano hiyo na kufuatilia mikanda ya mechi za wapinzani wetu kuhakikisha tunaenda kufanya vizuri," aliongeza Mgosi. Simba Queens imepangwa kundi A lenye timu za Lady Doves WFC ya Uganda na PVP FC ya Burundi.

Simba Queens ni Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania watawakilisha nchini katika michuano hiyo ya ukanda wa CECAFA na mshindi mmoja wa jumla kutoka makundi matatu, atafuzu kwenda nchini Misri kwenye michuano ya Ligi ya Mabigwa Afrika ya Wanawake.




Mkuu wa Kitengo cha Mauzo Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Abel Kaseko (kulia), akimkabidhi vifaa vya michezo Mwenyekiti wa Michezo Kanda ya Ngome, Kanali David Mziray, ikiwa ni msaada wa benki hiyo kwenda kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya michezo mbalimbali ya majeshi yanayotarajiwa kuanza Agosti 4, mwaka huu jijini Dodoma. Hafla ya makabidhiano hayo imefanyika leo jijini Dodoma. Wanaoshuhudia ni maofisa wa benki hiyo pamoja na maofisa wa Jeshi la Wananchi. **PICHA: NBC**

# NBC yakabidhi vifaa vya michezo JWTZ

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashindano ya michezo mbalimbali ya majeshi yanatarajiwa kuanza Agosti 4, mwaka huu jijini Dodoma, Benki ya NBC imetoa msaada wa vifaa vya michezo kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ili kusapoti jitihada katika sekta ya michezo.

Vifaa hivyo zikiwamo viatu vya michezo, mipira, jezi pamoja na vifaa vingine vya michezo mbalimbali vilikabidhiwa kwa Mwenyekiti wa michezo Kanda ya Ngome, Kanali David Mziray, na Meneja wa NBC tawi la Dodoma, Happiness Kizigira.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, Kanali Mziray alisema vitasaidia kuongeza hamasa kwa wachezaji wa timu za JWTZ ambao wamepania kuchukua vikombe mbalimbali vya mashindano hayo.

"Kwa kupata vifaa hivi kutawasaidia wachezaji wetu kuongeza hamasa zaidi kwenye mashindano hayo ambayo timu zetu zimepania kunyakua makombe yote," alisema Mziray.

Naye Meneja wa NBC tawi la Dodoma, Kizigira alisema wametoa vifaa hivyo kutokana na kuwapo na ushirikiano mzuri kati ya benki hiyo na Jeshi la Wananchi.

"Benki ya NBC tumekuwa na mahusiano mazuri ya muda mrefu na Jeshi la Wananchi na kwa kuwa mwezi ujao wenzetu watakuwa na jambo lao hapa Dodoma ambalo kimsingi tunawaombea mafanikio sana, tumeona ni vema tuwaunge mkono ili mambo yaende vizuri zaidi," alisema Kizigira.

Kizigira alisema vifaa hivyo wamevitoa Makao Makuu ya Jeshi kwa lengo la kuweza kuwafikia wanamichezo wote wa jeshi hilo ambao watashiriki mashindano hayo mwaka huu.

# Mihogo Festival yakusanya wasanii kibao

**Na Sabato Kasika**

WAIMBAJI mbalimbali wa muziki wa dansi, taarab, singeli na bongofleva, walitoa burudani katika tamasha liitwalo Mihogo Festival, lililofanyika juzi kwenye ufukwe kwa Coco, jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya waimbaji hao ni Mwinjuma Muumin (dansi), Nay wa Mitego (bongofleva), MC Kinata (singeli) na Safina (taarab), ambao walipagawisha mashabiki waliofika kushuhudia onyesho hilo.

Akizungumzia tamasha hilo, mratibu wake Reuben Ndege, alisema lililenga kuhamasisha vijana katika biashara ya mhongo, kuanzia kulima na kuuza ndani na hata nje ya nchi kwa vile zao hilo kwa sasa lina soko.

"Tumekuwa tukitumia wasanii mchnganyiko katika matamasha, kwa kuwa wana mashabiki wao wakiwamo wafanyabishara kama hawa waliopo Coco Beach ambao wanafanya biashara ya kukaanga mihogo," alisema.

Alisema, kwa muda mrefu wamekuwa wakizunguka ndani na nje ya jijiji la Dar es Salaam wakihamasisha vijana, akina mama katika kujishughulisha na kwa ajili ya kujiletea maendeleo, wakitumia kaulimbiu ya 'Mchongo mzima.

Kwa upande wake mwimbaji Mwinjuma Muumin, alisema yeye ni miongoni mwa waimbaji wa muziki wa dansi ambao wamekuwa wakishiriki mata,asha hayo likiwani la kilele cha maadhimisho ya vibonzo duniani.

"Maadhimisho hayo yalifanyika mwezi uliopita kule Buza, nilitumia nafasi hiyo kutambulisha wimbo wangu wa 'Kwa mpangarange Sihami', na ninaendelea kutambulisha zaidi kadri inavyowezekana," alisema Muumin.

Mkongwe huyo wa muziki wa dansi alisema, hatua ya kuitwa kwenye matamasha hayo inaonyesha wazi kuwa bado anakubalika ingawa baadhii ya watu wamekuwa wakidhani kuwa amechoka.

Alifafanua kuwa, kwa sasa ana nyimbo mpya sita za albamu ya kwanza akiwa na bendi yake ya Special Band ambayo alisema huenda ikazinduliwa rasmi Desemba mwaka huu iwapo mipango yao itakwenda kama walivyopanga.

# Biashara yaanza kujipanga kimataifa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Biashara United, umesema wiki ijayo utakutana na kocha wao, Patrick Odhiambo kwa lengo la kupanga mikakati yao kuelekea katika maandalizi ya mapema ya michuano ya kombe la Shirikisho Barani Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso alisema kikao hicho awali walitakiwa kukutana wiki iliyopita, lakini ilishindikana.

Alisema kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao ni nafasi nzuri kwao na wanahitaji kukutana na benchi la ufundi ili nkujadili mapendekezo yao ikiwemo usajili wa wachezaji wapya.

**"Tunahitaji kufanya usajili mzuri kwa lengo la kuboresha kikosi cha timu yetu kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kombe la Shirikisho," alisema Mataso**

"Tunahitaji kuwa makini katika usajili wa wachezaji wapya na maandalizi hayo yanaanza sasa kuhakikisha tunaboresha maboresha timu yetu, " aliongeza. Alisema nafasi hizi kwao ni muhimu na watapambana kuhakikisha muda huu wanaweka w mazingira mazuri ya timu yao.

Michezo
Jumatatu Julai 19, 2021
Nipashe



## Giroud: Nataka mataji na Milan

HABARI UK. 22




Wachezaji wa Simba wakishangilia na kombe lao baada ya kutangazwa kuwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, jana. PICHA: JUMANNE JUMA

# SIMBA YAPEWA MWALI BOCCO ATWAA KIATU

### ●●●Gwambina, JKT, Ihefu zashuka daraja, Costal vs Mtibwa kucheza mchujo...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya nne ya nyongeza lililofungwa na Nahodha wa Simba, John Bocco, limemfanya mchezaji huyo kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2020/21, huku timu yake ikiirarua Namungo FC mabao 4-0 kwenye mechi ya kumaliza msimu, ikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Saalam.

Wakati Simba ikikabidhiwa kombe baada ya kutwaa ubingwa msimu huu, timu za Ihefu FC, Gwambina na JKT Tanzania zimeungana na Mwadui kushuka daraja kutoka Ligi Kuu hadi Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Timu za Coastal Union na Mtibwa Sugar sasa zitasubiri majaliwa yao kwenye mechi za mchujo, zitakapocheza na timu za daraja la kwanza, ambapo zitalazimika kushinda ili kubaki Ligi Kuu, lakini kama zikipoteza zitakwenda daraja la kwanza.

Bocco aliyeingia mwishoni mwa kipindi cha pili, aliangushwa ndani ya hatari na mwamuzi kuamuru mkwaju wa penalti, ambapo yeye mwenyewe aliujaza wavuni na kufikisha mabao 16.

Kabla ya hapo, Chriss Mugalu alikuwa amefunga mabao mawili kwenye mechi hiyo na kufikisha jumla ya mabao 15 sawa na Bocco, kabla ya nahodha huyo kuandikisha bao lililomfanya kutwaa kiatu cha dhahabu kwa mara ya pili tangu aanze kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2008/09.

Akiwa Azam FC, Bocco alikuwa mfungaji bora, msimu wa 2011/12, alipomaliza akiwa amepachika mabao 19.

Bao lingine la Simba lilifungwa na Meddie Kagere ambaye ndiye alianza kufungua akaunti ya mabao kwa Simba dakika ya 18, kabla ya Mugalu kufunga mawili dakika ya 25 na 67, Bocco akipigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Namungo.

Katika mechi zingine za kufunga msimu wa ligi, Yanga, ikiwa ugenini, ililazimishwa suluhu dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Polisi Tanzania ikachapa Mwadui bo 1-0, huku Azam ikiidungua Ruvu Shooting bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Ihefu, timu iliyopanda daraja msimu huu, imerejea ilikotoka baada ya kuchapwa bo 1-0 dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, huku timu nyingine iliyopanda daraja msimu huu, Gwambina FC nayo ikishuka baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Prisons, Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga.

**Licha ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, JKT Tanzania, timu ya muda mrefu kwenye Ligi Kuu, imeshuka daraja baada ya kushika nafasi ya 15 na kuwa sawa na Mtibwa kwa pointi 39, lakini ikaponzwa na uwiano mbovu wa mabao ya kufungwa.**

Mtibwa ikaponea chupuchupu kwani pamoja na kupoteza mechi hiyo, ikaangukia kwenye nafasi ya 14 na sasa itakwenda kucheza mechi ya mchujo kuamua kama itabaki, au itashuka.

Ushindi wa mabao 3-1 iliyoupata Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga dhidi ya Kagera Sugar, umeifanya timu hiyo nayo kunusurika kushuka na sasa itakwenda kucheza mechi ya mchujo.

Pamoja kupoteza mechi hiyo, Kagera Sugar imepona na kubaki Ligi Kuu, baada ya kuangukia kwenye nafasi ya 12.

Mbeya City, timu nyingine iliyokuwa kwenye hatari ya kushuka, imebaki Ligi Kuu, baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya na kukamata nafasi ya 10.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >